Hakimiliki © 2007-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

# MSAMAHA NA UPATANISHO

**na**

**Jonathan M. Menn**

**B.A., Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., Cornell Law School, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders-East Africa**
**3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914**
**(920) 731-5523**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

Mei 2007; toleo jipya Mei 2013; imesahihishwa Julai 2014; imesahihishwa Novemba 2017

Msamaha na upatanisho ni moyo wa huduma ya Kristo, ni inapaswa kuwa moyo wa jinsi tunavyowatazama wengine. Kozi hii inashughulika na misingi muhimu ya kimaandiko kuhusu msamaha na upatanisho. Inajadili maana na kile ambacho si maana ya msamaha na upatanisho na tofauti kati ya msamaha na upatanisho. Sababu halisi za kujadili msamaha na upatanisho na mifano halisi ya jinsi ya kusamehe na kupatanisho zimehusishwa. Pia uhusiano kati ya msamaha na toba na jambo la kujisamehe binafsi nalo limefanyiwa kazi humu.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

**MSAMAHA…....……………………………………………………………………………………………2**

**Rejea za Maandiko Muhimu……………………………………………………………........................2**
**I. Msamaha ni sehemu halisi ya asili ya Mungu ……………………….………………………….......2**
**II. Tumeamriwa na Kristo--kama kiini cha maana ya kuwa Mkristo—kusamehe wengine. ……….…..3**
**III. Mitume hutueleza sisi kuwasamehe wengine, kama sheria na kuonyesha kielelezo…...........................4**

**Kuelewa na Kutumia Msamaha katika maisha yetu……. ……………………………….................5**
**I. Nini SI msamaha………..……………………………………………..............................................5**
**II. Msamaha NI nini…………..………………………………………………………………...........9**
**III. Sababu za kivitendo zinazoeleza kwa nini tuwasamehe waliotukosea…..……….................................10**
**IV. Jinsi ya kusamehe……………………………………………………………………………….12**
**V. Kujisamehe mwenyewe…………………………………………………………………………...17**
**VI. Toba na Msamaha……………………………………………………………………….......…18**
**VII. Kupokea msamaha kwa ajili ya dhambi zetu tulizomkosea Mungu na watu wengine.………………22**

**UPATANISHO………………………………………………………………………...….........26**

**Rejea Muhimu za Maandiko………………………………………………………………….…..........26**
**I. Mungu ametupatanisha sisi na nafsi yake mwenyewe na kutupa huduma ya upatanisho (2 Wakor 5:16-21)…………………………………………………………………………...26**
**II. Mungu amemaliza vikwazo vyote vinavyozuia upatanisho hata kati ya watu waliotofautiana sana (Waef 2:11-22)…...........………………………………………………………………....26**
**III. Kupatanishwa kwetu mmoja kwa mwingine ni muhimu kiroho na kunahusiana na kumwabudu kwetu Mungu (Math5:21-22)………..…………………………………….….........27**
**IV. Wakristo wameagizwa na Kristo na mitume wafanye kila wawezalo kuishi kwa amani wao kwa wao na pamoja na watu wote..…………………………………………………...…....28**
**V. Kristo na Mitume walidhihirisha upatanisho kwa vitendo kwa maisha yao wenyewe…......................28**
**VI. Tunaposhindwa kutatua mgogoro sisi wenyewe , Mungu analiagiza kanisa liingilie na kuleta hekima, rasilimali na mamlaka yake ili kushughulikia tatizo (Math 18:16-17; Wafil 4:2-3; 1 Wakor 6:1-8)……………………………………………………………………………..28**

**Kuelewa na Kutumia Upatanisho katika Maisha Yetu…….………………………….................29**
**I. Tofauti kati ya msamaha na upatanisho…………………………….................................................29**
**II. Kwa nini upatanisho una umuhimu wa kibusara……………………………………….……29**
**III. Jinsi ya kupatanisha…………………………………………………….........................30**

**NUKUU ZILIZOTUMIKA……..………………………………………………………………...33**

**NYONGEZA: Mfano wa Msamaha wenye msingi wa maamuzi kwa ajili ya urejesho wa Ndoa na Mahusiano ya Kifamilia…..………….......................................................................................34**

**MWANDISHI…..………………………………………………..……………………..37**

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

# MSAMAHA

## Rejea za Maandiko Muhimu[1]

## I. Msamaha ni sehemu halisi ya asili ya Mungu

**A.** ***Msamaha ni kiini cha asili na tabia ya Mungu***

**1.** Mungu mwenyewe anatangaza hivi: [6] *Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; 7 mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne."* (**Kutoka 34:6-7**)

**2.** Hili lilitambuliwa na wengine: (**Hesabu14:17-19; Zab 103:2-3;** na **Zab 130:3-4**).

**3.** Msamaha wa Mungu kwa dhambi zetu unadhihirisha uaminifu wake kwetu: *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeyeni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."* (**1 Yoh 1:9**).

**B.** ***Msamaha ni sehemu ya asili na utume wa Yesu Kristo***

**1.** Kristo mwenyewe alitangaza kwamba ana mamlaka ya kusamehe dhambi za watu: [3] *Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne.* [4] *Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo; na wakiisha kuivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza.* [5] *Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.* [6] *Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao,* [7] *Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?* [8] *Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu?* [9] *Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende?* [10] *Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza),* [11] *Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako.* [12] *Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe."* (**Marko 2:3-12**) Mengine yanayofanana na tukio hili ni **Math 9:2-8** na **Luka 5:17**-26. Tazama pia **Luka 7:48-50:** Mamalaka ya Kristo yalionekana na wengine; **Luka 23:33-34:** Kristo alisamehe wengine hata akiwa msalabani.

**2.** Msamaha wa Kristo kwa dhambi za watu ni kiini cha utume wake duniani; na inaenda sambamba na umuhimu wa Injili, iliyotangazwa na mitume, na inapaswa kutangazwa na sisi:

**a. Matendo 5:29-32:** [29] *Petro na mitume wakajibu, wakisema, "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.* [30] *Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti.* [31] *Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.* [32] *Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio."*

**b. Matendo 13:36-39:** [36] *Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.* [37] *Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.* [38] *Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;* [39] *na kwa yeyekila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa..*

**c. Wakol 1:13-14:** [13] *Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;* [14] *ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi.*

**d.** Tazama pia: **Luka 24:46-47; Matendo 2:38; 10:43; 13:38-39; 26:15-18; Waef 1:7; 1 Yoh 2:12.**

[1]Nukuu zote za Biblia zimetoka katika toleo la New American Standard ikiwa vinginevyo imeelezwa.

**II. <u>Sisi Tumeagizwa na Kristo—kama kiini cha maana ya kuwa Mkristo—kusamehe wengine</u>**

**A.** ***Sala ya Bwana inatutaka sisi kusamehe wengine kama sisi tulivyosamehewa:*** *[9] Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe.[10] Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. [11]Utupe leo riziki yetu. [12]Utusamehe deni zetu,kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. [13]Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina. [14]Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. [15]Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.* (**Math 6:9-15**) Kifungu kinachofanana na hicho ni **Luka 11:2-4**.

**1.** Zinagatia kwamba sehemu ya sala ya Bwana ambayo Yesu alisisitiza kipekee na kupendekeza ni sehemu ya maombi inayohusu kusamehe.

**2.** Zingatia kwamba kutokusamehe pia ni dhambi.

**3.** <u>Zingatia hatimaye kuwa Yesu ameweka wazi kabisa kwamba msamaha wa Mungu kwetu unategemeana sana na msamaha wetu kwa wengine:</u> Mungu atatusamehe sisi ikiwa sisi tutawasamehe wengine; lakini Mungu hatatusamehe sisi kama hatutawasamehe wengine. Kama D. A. Carson anavyoeleza kuwa: "Watu hujikosesha haki wenyewe ya kusamehewa kama wakiwa wagumu katika kung'ang'ania uchungu kiasi kwamba hawawezi au hawapo tayari kusamehe wengine. Katika hali hizo, hawaonyeshi kuvunjika, toba, hawatambui thamani kuu ya msamaha, hawana uelewa wa hali zao mbaya za dhambi, hawana toba" (Carson 2002: 79)[2]

**B.** ***Mfano mrefu sana wa Mathayo[3] ni juu ya umuhimu wa kusamehe wengine:*** *[21] Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? [22] Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini. [23] Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. [24] Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta [25] Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe,yeyena mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. [26] Basi yulemtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia. [27] Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni. [28] Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari [29] Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. [30] Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. [31] Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka. [32]Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi; [33] nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe? [34] Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote. [35] Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake."* (**Math 18:21-35**)

**C.** ***Yesu mfano wake mrefu kuliko yote ni katika Luka (na katika Biblia)ni juu ya msamaha na urejesho:*** *[11] Akasema, Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; [12] yule mdogo akamwambia babaye, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. [13] Hata baada ya siku si nyingi,yulemdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati.*
*[14] Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. [15] Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe.*
*[16] Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu.*
*[17] Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. [18] Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; [19] sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako.*
*[20] Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. [21] Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. [22] Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; [23] mleteni ndama yule aliyenona*

---

[2] Randy Alcorn analiweka hivi: "Hatumwumizi yeyote kupitia uchungu kwa kiwango ambacho tunajiumiza wenyewe. Mtu Fulani aliniambia, 'Uchungu ni sawa na kunywa sumu na kungoja mtu mwingine afe.'" (Alcorn 2009: 425)

[3] Mfano wa Yesu kuhusu watumwa wawili (**Math 18:21-35**) una maneno 245 katika kifungu cha kiyunani, ikihusisha swali la Petro la kwamba mara ngapi tuwasamehe wengine wanaotukosea, Nini tukio la mfano, na maneno yanayotambulisha mfano wa Yesu, "Yesu akamwambia." Mfano wa pili wa Yesu kwa urefu, wafanyakazi katika shamba la mzabibu (**Math 20:1-16**), una maneno 241 maneno ya kiyunani (yakihusishwa maneno mawili ambayo asili yake inatiliwa mashaka sana); ingawa maneno hayo yote, ni maneno ya Yesu mwenyewe. (Aland, et al.: 2001)

*mkamchinje; nasi tule na kufurahi; [24] kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia. [25] Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. [26] Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, Mambo haya, maana yake nini? [27] Akamwambia, Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima. [28] Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. [29] Akamjibu baba yake, akasema, Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwanambuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; [30] lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona. [31] Akamwambia, Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. [32] Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana'"* (**Luka 15:11-32**)

**D.** ***Yesu anaunganisha msamaha wetu na upendo wetu:*** *[36] Mtu mmoja katika Mafarisayo alimwalika ale chakula kwake; akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani. [37] Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya marimari yenye marhamu. [38] Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusubusu miguu yake na kuipaka yale marhamu. [39] Basi, yule Farisayo aliyemwalika alipoona vile, alisema moyoni mwake, Mtu huyu kama angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, naye ni wa namna gani, ya kwamba ni mwenye dhambi. [40] Yesu akajibu akamwambia, Simoni, nina neno nitakalo kukuambia. Akasema, Mwalimu, nena. [41] Akasema, Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili; mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini. [42] Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili.Katika hao wawilini yupiatakayempenda zaidi? [43] Simoni akajibu akasema, Nadhani ni yule ambaye alimsamehe nyingi. Akamwambia, Umeamua haki. [44] Akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simoni, Wamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu; bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. [45] Wewe hukunibusu; lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu yangu. [46] Hukunipaka kichwa changu mafuta; bali huyu amenipaka miguu yangu marhamu. Luka 7 [47] Kwa ajili ya hayo nakuambia, Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana; lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo. [48] Kisha alimwambia mwanamke, Umesamehewa dhambi zako. [49] Ndipo wale walioketi chakulani pamoja naye walianza kusema mioyoni mwao, Ni nani huyu hata asamehe dhambi? [50] Akamwambia yule mwanamke, Imani yako imekuokoa, enenda zako kwa amani.* (**Luka 7:36-50**)

**E.** ***Yesu anaunganisha kipekee kusamehe kwetu wengine na maisha yetu ya maombi na msamaha wa Mungu kwetu:*** *[23] "Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. [24] Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. [25] Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. [26] Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu."* (**Marko 11:23-26**)

**1.** Zingatia kuwa Yesu alitoa tamko hili wakati alipoingia Yerusalemu kwa shangwe, muda mfupi kabla ya kusulubiwa kwake. Ingawa yote aliyoyasema Yesu ni muhimu, maneno yaliyosemwa wakati kifo kinamfikia mtu yana umuhimu unaozidi.

**2.** Zingatia pia kwamba Yesu aliyarudia maneno aliyoyasema aliposisitiza na kushauri juu ya umuhimu wa msamaha katika sala ya Bwana. Matamko yanarudiwa kwa kusudi la kutilia mkazo umuhimu wake.

## III. Mitume hutueleza sisi kuwasamehe wengine, kama sheria na kuonyesha kielelezo

**A.** ***Paulo anatuagiza kusamehe:*** *Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.* (**Waef 4:32**; tazama pia **2 Wakor 2:7; Wakol 3:13**)

Maoni ya Carson kuhusu mstari huu: "Wazo si kwamba sisi tumesamehewa, na kwa hiyo tunatakiwa kusamehe, lakini kwamba Mungu mwenyewe, katika Kristo, ametusamehe, na kwa hiyo deni letu halipimiki. Haijalishi ni ubaya mkubwa kiasi gani tuliofanyiwa, ni kidogo ukilinganisha na uovu tuliofanya mbele za uso wa Mungu. Pamoja na hayo Mungu katika Kristo akatusamehe sisi. Ikiwa tunajua chochote kitupasacho kutoa msamaha, ikiwa tumevumbia chochote kuhusu ukubwa wa deni tunalowiwa na Mungu, sisi kuwasamehe wengine hakutakuwa jambo gumu." (Carson 2002: 80-81)

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**B.** ***Aina ya msamaha wa Paulo:*** *[10] Lakini kama mkimsamehe mtu neno lo lote, nami nimemsamehe; kwa maana mimi nami, ikiwa nimemsamehe mtu neno lo lote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo, [11] Shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake.* (**2 Wakor 2:10-11**)

**1.** Zingatia kuwa Paulo kuwasamehe wengine ni *kwa ajili ya kanisa* ("kwa ajili yenu"). Zaidi, mara zote alijua anachofanya (i.e., ikiwa anasamehe au hasamehi) hayo yanafanyika "katika uwepo wa Kristo."

**2.** Zingatia pia kwamba *kutosamehe* kutamfanya shetani "atushinde sisi."

**3.** Kilicho kweli kwa Paulo ni kweli kabisa kwetu, hasa sisi ambao (kama Paulo) tupo kwenye nafasi ya uongozi wa kanisa:

**a.** *Ikiwa tunasamehe au hatusamehi kanisa linaathirika kwa wema au kwa ubaya .*

**b.** *Ingawa hatumwoni yeye wala hatumhisi, kila tufanyacho (ikiwa ni pamoja na kusamehe au kutokusamehe ubaya uliotendwa dhidi yetu na wengine) kinafanyika katika uwepo wa Kristo*—na tutahukumiwa na Kristo ikiwa hatusamehi.

**c.** *Kutokusamehe kwetu kunampa shetani fursa na faida ya kufanya kazi kupitia sisi, na kinyume chetu, ndani na kinyume cha kanisa.* Kutosamehe kwetu kutasababisha wengine kufuata mfano wetu mbaya na kutosameheana—kanisa kwa njia hiyo litakuwa na mgawanyiko, litagawanyika, na lenye uchungu; na katika hali hiyo shetani peke yake tu ndiye anayefanikiwa. Kwa upande mwingine, kama tutakuwa na roho ya msamaha, washirika kanisani watafuata mfano wetu. Ikiwa tunasamehe tutaweza kuhubiri vifungu vyote vya Biblia kwa nguvu za Roho Mtakatifu, bila ya kuwa wanafiki. Katika hali hii, shetani hatapata fursa na faida ya kufanya kazi kupitia sisi au kupitia kanisa.

**C.** ***Stephano, shahidi wa kwanza wa kanisa, ametupa mfano mkuu (baada ya Yesu mwenyewe), kwa kuwasamehe wale waliomwua, hata wakati anakata roho:*** *[59] Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, "Bwana Yesu, pokea roho yangu." [60] Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala." Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.* (**Matendo 7:59-60**)

## Kuelewa na Kutumia Msamaha katika Maisha Yetu

### I. Nini SI msamaha[4]

**A.** ***Msamaha SI "kuita ubaya wema," kupunguza maumivu, kuvumilia ubaya, kusema "ulichofanya si kikubwa sana," au "si kitu," au kuwa na "kutokujali" kuhusu ubaya au kwa aliyefanya ubaya***

**1.** Msamaha ni kutambua kwamba alichotufanyia mtu mwingine NI ubaya. Hakika, kile alichofanya mtu mwingine ni kibaya sana hata Yesu akawa radhi kuteswa na kuawa kwa dhambi hiyo hiyo (vile vile kama kwa dhambi zetu zilivyo mbaya).

**2.** Kusema kuwa ubaya ni wema, au "si jambo la kutilia maanani," au "hakuna shida" ni kuacha *kweli*—kwa hiyo inatutenga sisi kutoka kwa Mungu na Kristo, kwa sababu Mungu ni kweli (**Kutoka 34:6; Zaburi 25:5, 10; 33:4; 40:10-11; 43:3; 57:10; 86:15; 89:14; 117:2; 119:142, 151; 138:2; Isaya 65:16**); Kristo ni kweli (**Math 22:16; Marko 12:14; Yoh 1:14, 17; 3:21; 8:45-46; 14:6; 18:37; Waef 4:21**); na sisi tunategemewa kuwa wakweli kwetu sisi wenyewe, mbele za Mungu na kwa wengine (**Zaburi 51:6; 86:11; 145:18; Mithali 3:3; 16:6; 23:23; Yoh 4:23-24; Waef 4:25**).

**3.** Msamaha si kuvumila. Tunapomsamehe mtu haimaanishi tunavumilia kile alichofanya, au tunamkaribisha atuumize tena, au tunataka itokee tena. Msamaha unahitaji jicho la wazi kujua tofauti kati ya wema na ubaya, na kuayaita mambo vile yalivyo,-kwa sababu unaweza tu kusamehe "ubaya" mkubwa unaoweza kukuumiza.

**B.** ***Msamaha SI udhaifu-kusamehe hakumaanishi kuwa unapoteza "utu" wako au "ubinadamu" wako***

**1.** Kumsamehe mtu fulani kwa ubaya aliokufanyia ni moja ya mambo magumu uliyowahi kufanya katika maisha yako. Ubaya unapozidi kuwa mkubwa na wenye kuumiza zaidi, ndivyo inavyozidi kuwa vigumu kumsamehe aliyetenda ubaya.

**2.** Inahitaji *nguvu*—nguvu ya mwili, ya ufahamu, ya nia, ya *tabia*—ili kuweza kusamehe aliyekutendea ubaya uliokuumiza sana. Ingawa, Yesu ametupa Roho Mtakatifu; tuna nguvu zake za kuweza kusamehe, kama vile ambavyo Yesu mwenyewe alivyotusamehe sisi(na wengine) kwa dhambi zetu na

[4] Hii sehemu kwa ujumla imezingatia kwa Jeffress 2000: sura za. 3 na 7; Smedes 1984: sura ya. 5; Smedes 1996: sura. 2-3; Enright 2001: sura. 2; na Klassen n.d.: "Definitions."

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kwa kumwua yeye. Tunapokuwa watii kwa Mungu, katika kweli ya Neno lake, na katika nguvu ya Roho wake, atatupa sisi imani na uwezo wa kufanya jambo gumu, kwa sababu ni jambo sahihi- kusamehe wale waliotujeruhi na kutuumiza sana. (**Warumi 4:19-22; 14:4; 1 Wakor 10:13; Waef 3:20-21; 6:10-16; Waeb 2:18; 7:25; Yuda 24**).

**3.** Mtu anaweza kudhani msamaha unatoa wajibu *mkubwa sana* kwa aliyekosewa kuliko aliyekosa. Ingawa, Jeffress anaeleza: "Mungu hatuondolei majukumu kwa sababu hayatufurahishi au magumu. Kwa mfano, zingatia haya maneno maarufu ya Yesu ya hotuba yake ya mlimani:

> Mmesikia kwamba imenenwa, 'Jicho kwa jicho, na jino kwa jino.' Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la kushoto na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili. [**Math 5:38-41**]

Zingatia kwamba kila hali ambayo Yesu anaitaja hapa, haweki majukumu kwa mkosaji, lakini kwa aliyekosewa. Aliyekosewa anatakiwa kugeuza shavu lingine, atoe kanzu yake vile vile kama joho lake, na kwenda maili ya pili." (Jeffress 2000: 45; tazama pia Sande 2004: 148-49; na Worthington 2003: 68, "Hatusamehi kwa sababu ni rahisi, lakini kwa sababu ni haki na ni mwitikio kwa upendo wa Mungu na msamaha wake kwetu.")

**4.** Ikiwa unadhani kumsamehe mtu fulani aliyekukosea kunakuondolea "hadhi" au "utu," zingatia hili: Hilo ndilo unalowaza kuhusu Kristo? Je yeye kwa kiasi ameshuka "hadhi" kwa sababu amekusamehe *wewe*?

## C. *Kusamehe SI kusahau*

**1.** "Kusaha ni mchakato *usiotumia nguvu wala akili* unofanya jambo kutoweka kwenye kumbukumbu kutokana na muda kupita. Kusamehe ni mchakato *mtambuka*; unahusisha uchaguzi wa kudhamiria na tendo hasa la kujitoa." (Sande 2004: 206).

**2.** Huwezi kusamehe kile ambacho umesahau. Ingawaje, punde tu tunaposamehe *tunaweza* kusahau kwa sababu tumeponywa.

**3.** Baadhi ya vifungu husema Mungu "husahau" dhambi zetu (tazama **Zab 103:12; Yeremia 31:34; Mika 7:19**).

**a.** Mistari ile, kama rejea za Biblia kuhusu "macho" ya Mungu (**2 Nyakati 16:9**), "masikio" yake (**1 Pet 3:12**), "mikono" yake (**Kutoka 24:11**), na "miguu" yake (**2 Samweli 22:10**) ni "kumpa Mungu sifa za kibinadamu," bila shaka nayo ni, kujaribu kumwelezea Mungu asiye na mwisho kwa kutumia mifano ya mwanadamu aliye na mwisho. Haileti maana kuamini kwamba Mungu anayejua yote ghafla anapoteza kumbukumbu na kusahau kabisa kile kilichofanywa na viumbe vyake.

**b.** Kwa hakika, Biblia huweka wazi kwamba matendo yetu *yote*, na nia zetu, yote mabaya na mema, yatahukumiwa na Mungu na kuamua kuhusu thawabu yetu ya milele (**Math 16:27; Luka 8:17; 12:2-3; Warumi 2:1-16; 14:10-12; 1 Wakor 3:12-15; 2 Wakor 5:10; Ufunuo 20:11-15; 22:12**). Hii inaonyesha kwamba Mungu ni lazima aweke kumbukumbu ya matendo yetu ili atuhukumu kwa haki.

**4.** "Mistari ya Biblia inayoongelea Mungu kusahau dhambi inajaribu kuelezea msamaha wa Mungu wa kisheria kwa dhambi zetu. Tunapopokea msamaha wa Mungu hatupaswi tena kuogopa adhabu ya milele kwa ajili ya dhambi zetu." (Jeffress 2000: 129). Ukweli huu umeelezwa kwa wazi katika **Warumi 4:7-8** (ambayo inanukuu **Zab 32:1-2**): [7] *Heri aliyesamehewa dhambi, Na kusitiriwa makosa yake.* [8]*Heri Bwana asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila.*

Jeffress anaelezea: "Dhambi zetu zinatufanya wadeni kwa Mungu. Tunawiwa na Mungu kwa dhambi tulizomtendea. Lakini kifo cha Kristo kimelipa deni katika ule muamala ambao Paulo anaueleza kwenye Wakolosai 2:13-14: … akiisha kutusamehe makosa yote; akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani. Tunapokuwa Wakristo, anachukua deni analokudai, analigongomea msalabani, na kutangaza limelipwa lote.' Lakini ni rahisi *kusamehe* deni bila ya *kulisahau."* (Jeffress 2000: 130)

**5.** Kwa namna nyingine kusema Mungu "husahau" makosa yetu ni kusema kwamba yeye hisia yake kwetu ni kana kwamba hakumbuki. Au, "wakati Mungu anaposema kwamba hakumbuki tena dhambi zako' (**Isaya 43:25**), hasemi kwamba *hawezi* kukumbuka dhambi zetu. Bali, anaahidi kwamba *hatazikumbuka.* Anapotusamehe, anaazimia kutozitaja, kutozihesabu, au kutofikiri tena kuhusu dhambi zetu kamwe." (Sande 2004: 206)

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**D.** ***Kusamehe SI kujitetea***

**1.** Kujitetea ni kinyume cha kusamehe. Tuna *tetea* watu tunapotambua kwamba *hawapaswi* kulaumiwa kwa jambo walilofanya, au kwa matokeo mabaya yaliyotokea kwa bahati mbaya kutokana na matendo waliyotenda kwa nia njema; Tuna*wasamehe* watu tunapotambua kuwa wana*paswa* kulaumiwa kwa jambo walilofanya—jambo ambalo ni kosa na halina utetezi—yakiwemo yale matendo mabaya ambayo kwa hayo walilenga kutuumiza sisi.

**2.** "Msamaha unasema, 'wote wawili tunajua ulichofanya ni kibaya na ni bila kujitetea. Lakini kwa kuwa Mungu amenisamehe mimi, nami nakusamehe wewe.' Kwa sababu msamaha hushughulikia dhambi kiuhalisia, unaleta uhuru ambao hakuna kiwango cha kujitetea kinaweza kuutoa." (Sande 2004: 206-07)

**E.** ***Msamaha SI sawa na "kuwakubali watu"***

**1.** Tuna*wakubali* watu kwa *wema* wao; tuna*wasamehe* watu kwa yale *mambo mabaya* waliyotutendea *sisi.*

**2.** Msamaha unahitajika kwa *tendo baya.* Hawezi "kusamehe" "tabia" fulani mbaya ya mtu au "asili," zaidi ya tunavyoweza kusamehe kabila lao, jinsia, utaifa, au ukweli kwamba wao wanatumia mkono wa kushoto. Vilevile, "hatusamehi" kule kuwa na mawazo tofauti. "Tunasamehe" tu ubaya, tendo la dhambi lililotuumiza.

**F.** ***Msamaha hautoi nafasi ya "kupuuzia haki" na HAUTOI "uhuru" kwa watu kuendelea na dhambi zao, lakini si lazima uondoe matokeo yote ya ubaya***

**1.** *Msamaha* ni kwa ajili ya mahusiano binafsi na ni kwa ajili ya kuponya majeraha ya ndani yako mwenyewe ambayo yametokana na ubaya uliofanyiwa-msamaha ukitumiwa kivitendo, ni jambo tunalofanya ndani ya mioyo yetu, ufahamu na nafsi. Unafanyika kwa kumtii Kristo, na kimsingi unaleta *uponyaji wetu wenyewe. Haki* katika jamii ni wajibu wa raia na mfumo wa makosa ya kijinai na ni kwa kusudi la kurekebisha uovu unaotendwa dhidi ya jamii. Sisi kuwasamehe wengine haimaanishi wao hawana "hatia" na inaweza isikubalike kisheria; haiondoi au haipo juu ya adhabu za kimahakama za mfumo wa nchi wa haki za raia na makosa ya kijinai, kwa sababu ubaya uliotendwa dhidi yetu unaweza kuwa ni ubaya unaoathiri nchi, na jamii au binadamu kwa ujumla.

**2.** Unasamehe uovu uliotendewa *wewe;* huwezi kusamehe mtu kwa ubaya aliofanya kwa mtu mwingine, au uliofanywa dhidi ya nchi au wanadamu kwa ujumla-huko ni *kuachilia.* Mtu akimwumiza mtoto wangu, hilo linaweza likaniumiza mimi pia, kwa sababu nampenda mtoto wangu. Ninaweza kumsamehe aliyetenda kosa nisiwe na hasira dhidi yake, nisiwe na uchungu na maumivu mengine ambayo yamenipata kutokana na alichofanya kwa mtoto wangu, lakini siwezi kumsamhe mkosaji *kwa niaba ya mtoto wangu* kwa kosa lililofanyika *kwa mtoto.* Mtoto wangu mwenyewe atapaswa kupitia mchakato wa kumsamehe mkosaji kwa kosa alilofanya kwake.

**3.** Uelewa kuhusu matokeo ya dhambi unatakiwa utusaidie kuelewa kwa nini sisi ni wenye dhambi wabaya zaidi kuliko tunavyojiona-dhambi moja huathiri watu wengi zaidi ya vile tunavyoweza kuwaza. Hiyo ndiyo sababu tunamhitaji *Kristo* atusamehe *sisi*—kwa sababu alizichukua dhambi zetu *zote* juu ya nafsi yake mwenyewe. Tunapotambua kina cha dhambi zetu, na kiwango cha msamaha wa Kristo kwetu, tunapaswa kuwa wepesi kuweza kusamehe wengine kwa makosa waliyotutendea.

**4.** Mwisho, Haki itapatikana kwa Mungu katika hukumu yake ya mwisho; huo si wajibu wetu. Sisi tukimsamehe mkosaji hiyo haimwondolei hatia yake mbele za Mungu na haibadilishi haki ambayo Mungu atatoa katika hukumu ya mwisho.

**5.** Msamaha haupunguzi ubaya wa matendo mabaya.

**a.** *"Hakuna msamaha halisi bila ya kuwepo kwanza kwa uwazi na ukweli wa hukumu" (Smedes 1984: 79).* Kila mtu anahisi maumizi yeye binafsi; kiwango cha maumivu yake hakiongezeki kwa sababu mtu ameumiza jozi, au mamia, au maelfu au hata mamilioni ya wengine—kila mwathirika anahisi kwa kipimo kilichojaa cha maumivu yake hata kama mamilioni wengine wameumizwa.

**b.** *Kusema kwamba baadhi ya "majitu" hawasameheki inashangaza inawafanya wawe vile wanavyotaka inawainua na kuwafanya—inawainua kuwa "binadamu wa ajabu" wenye hadhi, kama ya shetani.* Cha kushangaza, hilo linawatoa katika kuhitaji msamaha, au kutoka kwenye wajibu wa kibinadamu, kwa sababu wao ni zaidi ya binadamu. Hii inasababisha mtazamo uliopotoka kwamba waathirika ni lazima waishi na siku zote na majeraha yao na maumivu, kwa sababu kamwe hawataponywa majeraha kupitia msamaha. Kwa kuwaona "majitu" (wauaji wa halaiki, waasi wa kisiasa katika historia, nk.) kana kwamba kwa kiasi fulani ni "tofauti" na sisi

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wengine wote, "wakubwa" kuliko sisi, inatufanya tuwe wadogo na ni kinyume na kweli. Ukweli ni kwamba "watu wa kawaida sana hufanya ubaya usio wa kawaida" (Smedes 1984: 81).

**c.** *Mwandishi wa Kirusi Aleksandr Solzhenitsyn alivumbua:* "Kama tu ingelikuwa rahisi! Kama kungekuwa na watu wabaya mahali fulani kwa siri wakitenda mabaya, ingekuwa lazima kuwatenga na sisi tuliobaki na kuwaangamiza. Lakini mstari unaotenga kati ya ubaya na wema hupita katikati ya moyo wa kila mwanadamu. Na ni nani aliye tayari kuangamiza kipande cha moyo wake mwenyewe?" (Solzhenitsyn 1985: 75)

**6.** Unapomsamhe aliyekukosea na kukuumiza, unachofanya si lazima kiondoe matokeo ya makosa kwa *mkosaji.*

**a.** *"Matokeo ya kiasili ya matendo yamepangwa vizuri na Mungu na yanatufanya tuwe watu ambao tunatakiwa kuwa. Kuyapunguza makali inaweza kuwa ni kuwaumiza wale ambao walikusudiwa kusaidika."* (Willard 1997: 262) Kwa mfano, Daudi alipofanya uzinzi na Bathsheba na kusababisha mume wake Uria Mhiti kuawa, ingawa Mungu alimsamehe Daudi dhambi yake, hata hivyo Mungu alieleza kwamba: *"upanga hautaondoka nyumbani mwako . . . Nitakuondokeshea uovu katika nyumba yako, nami nitawatwaa wake zako mbele ya macho yako, na kumpa jirani yako, naye atalala na wake zako mbele ya jua hili. Maana wewe ulifanya jambo lile kwa siri; bali mimi nitalifanya jambo hili mbele ya Israeli wote na mbele ya jua. [na] kwa kuwa kwa tendo hili umewapa adui za Bwana nafasi kubwa ya kukufuru, mtoto atakayezaliwa kwako hakika yake atakufa."* (**2 Samweli 12 7-14**)

**b.** *"Mkosaji hayupo 'nje ya ndoano' tunaposamehe; tunagundua kwamba 'sisi tunakuwa nje ya ndoano' tunaposamehe"* (Klassen n.d.: n.p.). Anaongeza, "Ninaposamehe ninamweka mfungwa huru na hapo ninagundua kwamba mfungwa ni mimi" (Ibid.).

**7.** Vivyo hivyo unapomsamehe mtu aliyekukosea na kukuumiza, siyo lazima matokeo ya lile kosa ulilotendewa yaondoke *kwako.* Kwa mfano, "Ninaweza kumsamehe mtu aliyenipofusha, lakini kusamehe kwangu hakutanirudishia kuona" (Klassen n.d.: n.p.). Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba, ingawa "kusamehe hakuondoi maumivu . . . msamaha hutusaidia sisi *kuchukuliana* na maumivu" (Ibid., anasisitiza na anaongezea). Zaidi, Mungu *hutumia msamaha* (ambao ni utii wetu kwake) kutubadilisha sisi na kutufanya tuzidi kufanana na Kristo, kutuvuta karibu na yeye, na kutupa ufunuo, huruma na unyenyekevu. Katika mchakato (na unaweza kuwa mchakato mrefu—kwa hakika, mchakato wa maisha yote), tunapofikia kujua makusudi yake katika majeraha na kutenda kwake kazi katika maisha yetu kwa njia ya majeraha na kwa njia ya msamaha wetu, atabadilisha maumivu na kuyaondoa mbali.

**G.** ***Msamaha HAINA maana uendelee kumtumaini mkosaji, au kuendelea na urafiki, au katika mahusiano na yeye.***

**1.** Msamaha *unatolewa*; kuaminika *kunatafutwa.* Urafiki unahitaji kuaminiana na kuheshimiana kwa pande zote. Heshima, kama kuaminika, inatafutwa.

**2.** Anahitajika mtu moja ili kusamehe; Wanahitajika watu wawili ili kupatana. Msamaha ni jambo linalotokea ndani ya mtu anayefanya hivyo" (Smedes 1996: 25). Smedes anaongeza, "Tunasamehe ndani ya mioyo yetu na ufahamu wetu; yanayotokea kwa wale tunaowasamehe yanawategemea wao" (Ibid.: 177). Siyo jambo linalofanana na upatanisho, inagwa ni sehemu ya upatanisho—msamaha unatangulia upatanisho:

**a.** *Msamaha ni mwitikio wa kimaadili kwa mwingine aliyetenda kinyume na maadili.*

**b.** *Upatanisho ni kuja pamoja kwa watu wawili kurejesha mahusiano yaliyopoteza kuaminiana* (kuondoa kizuizi cha mahusiano mazuri).

**3.** Ni kweli tunapaswa *"kuwapenda adui zetu, kuwaombea wale wanaokuudhi"* (**Math 5:44**); *"wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale wanaowachukia ninyi"* (**Luka 6:27**); na *"wapendeni adui zenu, watendeeni mema"* (**Luka 6:35**). Yesu alisema kwamba amri ni, "*mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe,"* pamoja na kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, nafsi, na akili ni msingi kwa *"sheria yote na manabii"* (**Math 22:37-40**).[5]

**a.** *Zinagatia kwamba Yesu hakusema tunatakiwa "kuwakubali" adui zetu.* Alitambua kwamba kwa hakika kwamba, tutakuwa na maadui watakaotutesa. Hata hivyo tunatakiwa "kuwapenda"

---

[5]Rejea yake "Sheria yote na Manabii" anarejea *Biblia nzima* (Agano la Kale)—nayo ni., Neno lote la Mungu lililofunuliwa kwa ajili ya jinsi tunavyotakiwa kuishi. Paulo vilevile alisema, "Biblia nzima inatimizwa katika neno moja, katika tamko kwamba, 'Mpende jirani yako kama nafsi yako'" (**Wagal 5:14**). Tamko kwamba "mpende jirani yako kama nafsi yako" linatoka katika **Mambo ya Walawi 19:18**.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wao. Na tena aliongeza kwamba, "kama wewe utawapenda [tu] wale wanaokupenda, utapata thawabu gani? Je hata watoza ushuru hawatendi vivyo hivyo?" (**Math 5:46**)

**b.** *Maana na kusudi la upendo huo ni hii:* "Mtu kuwapenda jirani, adui zake . . . si lazima iwe ni kutenda kile kinachowapendeza, lakini ni kuchagua kuwaonyeshea upendeleo na nia njema . . . Mtu anatakiwa atambue uhitaji wa watu kubadilishwa kwa njia ya neema ya Kristo, na kufanya kila liwezekanalo ili kuwaleta katika maarifa ya Bwana. Hili linaweza kuhusisha matendo ya ukarimu au hata marudi na kunidhamisha, yote ikiwa ni kazi ya upendo. . . . Tukirejea upendo wa Mungu [ambao tunatakiwa kuuonyesha], ni mapenzi makamilifu ya Mungu kwa mwanadamu. Inahusisha utendaji wa Mungu wa yale anayojua kwamba ni mema kwa ajili ya mtu na siyo lazima yawe ni yale anayotamani mtu." (Zodhiates 1993: *agapáō; agápē*)

**c.** *Kwa hiyo, kupenda si kumchukia mkosaji, hata kama amekuumiza, bali kufanya kwa ajili ya usalama wake, kumwonyesha ukarimu na wema, kujitoa kibinafsi kama sadaka.* Kupenda kunahusisha kusamehe. Kupitia hili, Mungu anaweza kubalisha hisia dhidi ya mkosaji kwa kadiri anavyokubadilisha na kuondoa maumivu unayohisi kama matokeo ya kosa.

**d.** *Kumpenda adui au jirani yako haimaanishi umwache aendelee na njia yake, au umtumaini baada ya kumthibitisha kuwa hastahili, au uendelee naye katika biashara baada ya kumthibitisha kuwa ni mtu asiyejua biashara, au uishi naye hata kama yeye ananyanyasa au ni hatari kwako.* Kufanya hivi kungeendeleza hali ya dhambi ya mtu. Hiyo kwa hakika siyo kwa faida yake, na wala kuendeleza hali ya dhambi hakutamtukuza Mungu. Inawezekana kurekebisha mahusiano na kumpatanisha mtu—lakini kufanya hivyo kunakuhitaji *juhudi ya pamoja* kati yako na mwingine katika upatanisho, siyo tu wewe kumsamehe kwa lile baya alilofanya.

## II. <u>Msamaha NI nini</u>

### A. *Msamaha unaelezwa: Msamaha ni aina ya neema-ni kufutwa kwa deni*

Msamaha ni:

**1.** Kutambua kwamba kosa limetendeka;

**2.** Kutambua kwamba kosa lililofanyika limesababisha ulazima wa kulipiwa; na

**3.** Kuchagua kwa kujitolea kumwachilia mkosaji kutoka kwenye wajibu na kugharimikia hasara wewe mwenyewe (Jeffress 2000: 49; see also Willard 1997: 262, "Tunamsamehe mtu kwa kosa alilotufanyia tunapoamua kwamba hawatapata dhara lolote kwa kosa hilo kwa namna yeyote ile"). Kwa hiyo, msamaha ni aina ya neema. Neema ni uamuzi wa dhati *kutoa kitu kizuri* kwa mtu *asiyestahili*. Ni kama Mungu alivyoamua kukusamehe *wewe*. Usisahau kamwe kwamba wewe ulisamehewa *tu* kwa neema ya Mungu; wewe *hukustahili*.

### B. *Msamaha unafafanuliwa: Msamaha ni uzoefu wa kihisia ambao unahusisha utu wetu katika ujumla wake*

**1.** <u>Kila mtu ana utu ulio na mambo mengi ambao kwa kiwango cha chini angalau una sehemu kuu tatu za asili yake (ukiongezea kwenye mwili).</u> Hizo sehemu za mtu ni: (A) Uwezo wa *ufahamu* (nao ni., uwezo wa kufikiri, kuchambua, kujua, na kuelewa mambo); (B) Uwezo wa *Utashi* (nao ni., uwezo wa kufanya maamuzi na kufanyia kazi hayo maamuzi; matumizi ya nia); na (C) Uwezo wa *hisia* (nayo ni., kipengele cha hisia; uwezo wa" kuhisi"). Kama lengo la msamaha ni kuondoa deni, msamaha"wa kweli" na wa kudumu unaweza kutolewa tu ikiwa kutakuwepo na kuhusishwa kwa ukamilifu ufahamu, hisia na utashi katika mchakato wa kusamehe.[6]

**2.** <u>*Kutokusamehe* kunatokea wakati:</u> (A) Kosa linatokea; (B) Tunaliona kosa kama maumivu au kwazo; (C) Maumivu husababisha "joto" (ghafla) hisia za hasira na hofu(ya kuumizwa tena); (D) Baada ya muda katika fahamu zetu tunakumbuka na kuishi katika (nayo ni., tunacheua) kosa, mkosaji na makusudi yake, na matokeo ya kosa; (E) Hili linatupelekea kutosamehe, ambako kunahusisha "kupoa" (kukawia, muda mrefu) hisia za chuki, uchungu, mabaki ya hasira, mabaki ya hofu, uadui, na msongo. Hisia zenyewe ni zaidi ya "mihemko"; ni uzoefu wa mwili mzima unaohusisha ubongo, nyuroni, na nyurokemikali, misuli, homoni, na njia nzima ya chakula.[7]

---

[6]Worthington inaonyesha kwamba kuna msamaha aina mbili (au hata hivyo yaelezwa vizuri, namna mbili za kusamehe) (1) *msamaha kama uamuzi* ("msamaha wa kuamua"— "kuachilia deni"); na (2) *msamaha kama kuondoa maumivu ya ndani* ("msamaha wa mhemko") (Worthington, 2003: ch. 2).

[7]Hili na visehemu vidogo vinavyofuata viwili vipo kwa mujibu wa Worthington 2003: 30-45.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**3.** Kwa hiyo msamaha, siyo tu kufahamu na kutambua kwamba umekosewa na kuchagua kwa kukusudia kuachilia na kuchukua hasara mwenyewe. Badala yake, msamaha ni tendo la kumaanisha kutoka moyoni linalotambua kuwa kuumizwa isivyofaa na mtu mwingine kunasababisha maumivu ya kihisia ya ndani yanayotuathiri katika utu wetu wa ndani. Msamaha ni "uzoefu wa kihisia" kwa sababu ni *kubalishwa kihisia.* Msamaha unaondoa "hisia kali" (chuki, hasira, na woga), msamaha na "hisia baridi" (kukwazika, uchunga, masalia ya chuki, masalia ya hofu, ukatili, na msongo ambao ni matokeo ya kucheua kosa), kwa *kubadilishana* na "hisia chanya" kama vile upendo usio na ubinafsi, huruma na rehema kwa mkosaji.[8] Hii pekee "msamaha wa kihisia" kwa hakika "huponya moyo" (Worthington 2003: 44-45).
**4.** Tunaposamehe, tunaruhusu shauku ya kuzuia kulipa au kutafuta kumlipa kisasi mkosaji. Badala yake, msamaha hulipa jema kwa baya. Msamaha huyaondoa mawazo yasiyofaa, na mawazo yanayomtakia mabaya mkosaji na kuachilia mawazo yanayomtakia *mema* mkosaji. Hivyo, msamaha kwa hakika ni karama ambayo inabeba neema, upendo, na uhuru (huru kutoka utumwa wa chuki, hasira, hofu, mawazo mabaya, kuishi kwa mambo yaliyopita, kukaa kwenye makosa na maumivu). Tunatambua ya kwamba mkosaji hana haki kwa mambo hayo (kama vile ambavyo na sisi hatuna haki ya kusamehewa na *Mungu*).
**5.** Huwezi kisaikolojia ukapata *uzoefu* wa msamaha wa kweli—hata kama umesamehewa kweli-hadi hapo hisia zinapobadilika. Hata kama ukibadilisha fikra zako, mapenzi yako, na matendo yako, hutapata *uzoefu* wa msamaha mpaka hisia zako zibadilike—*lakini kubadilisha fikra zako mapenzi yako, na matendo yako lazima yakuongoze kufikia kubadilishwa kwa hisia zako*. "Msamaha hautaondoa kumbukumbu zinazoumiza; unaondoa hisia hasi" (Ibid.: 133).
**6.** Msamaha ni *fumbo*, kitu kama *"ni heri kutoa kuliko kupokea"* (**Matendo 20:35**) au *"akupigaye shavu lako la kuume mgeuzie la pili pia"* (**Math 5:39-42; Luka 6:29-30**). Kwa msamaha tunatambua kwamba: (A) kosa lilitokea ni baya na halikubaliki na siku zote litabaki kuwa baya na lisilokubalika: (B) tuna haki ya kimaadili ya kuwa na hasira; lakini (C) kwa hiari yetu tunaachilia hiyo "haki" yetu kama tendo la rehema na upendo, kama zawadi kwa mkosaji asiyestahili, kwa kumtii Kristo. Kwa hiyo fumbo: kuwa huru mbali na hasira na kukwazika, kunampa mtu aliyekukosea zawadi ya msamaha na kukuweka huru wewe mwenyewe.

## III. Sababu za kivitendo zinazoeleza kwa nini ni lazima tuwasamehe waliotukosea

### A. *Kusamhe ni wajibu kwa aliyesamehewa*[9]

**1.** "Katika Biblia nzima inaonekana hakuna kuachana kati ya kupokea na kutoa msamaha" (Jeffress 2000: 57). Hiyo ndiyo maana wote wawili Yesu katika sala ya Bwana (**Math 6:9-15**) na Paulo (**Waef 4:32**) wanatuamuru kusamehe.
**2.** Hata wapagani katika mfano wa watumwa wawili walitambua kuwepo kwa muunganiko kati ya kusamehewa na kusamehe wengine. Ndiyo maana "walichukizwa sana" wakati mtumwa aliyesamehewa nyingi na Bwana wake aliposhindwa kumsamehe mtumwa mwenzake aliyekuwa anamdai kiasi kidogo; hivyo, wakatoa taarifa ya kutosamehe huko kwa Bwana (**Math 18:31**).
**3.** Kusudi letu katika haya maisha ni "kufananishwa na mfano wa mwanawe" (**Warumi 8:29**), ni "kuwa wakamilifu kama Baba yetu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (**Math 5:48**). Kwa maana msamaha hugusa moja kwa moja moyo wa asili na utume wa Mungu na Kristo, msamaha wetu ni alama ya muhimu sana ya *kutakaswa* kwetu Ni ishara ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu ndani yetu akitubadilisha na kutufananisha na mfano wa Kristo na kutukamilisha. Hii ndiyo maana Kristo aliuunganisha msamaha na upendo (**Luka 7:36-50**) na pamoja na maombi (**Marko 11:23-26**). Kama asemavyo Carson, "Wale wajuao kuwa wamesamehewa ndiyo wale wanaosamehe. Moja ya alama ya kukua kiroho kwa mkristo, Whitney anaeleza, ni kwamba anakuwa 'mwepesi kusamehe.'" (Carson 2002: 80).
**4.** Msamaha si "jukumu" la kawaida lililo rahisi bali huhusisha mtazamo wa msingi wa maisha ya mtu-ambayo ni kwamba mtu kimsingi amejielekeza kwa Mungu na anaishi akimpendeza yeye na kufanana naye au vinginevyo.

**a.** *Hii inatumika hivyo hivyo kwa msamaha na upatanisho:* "Kumtazama Mungu ni ufunguo wa

[8] Smedes anaweka hivyo hivyo; misingi ya msamaha inahusisha hatua tatu: "[1] Tunatambua ubinadamu wa mtu aliyetuumiza sisi. [2] Tunatoa haki zetu ili kuzipata hata zaidi. [3] Tunafanya hisia zetu ziwe katika mtazamo wa Yule tunayemsamehe." (Smedes 1996: 6-12)
[9] Sehemu hii kwa ujumla ni kwa mujibu wa Jeffress 2000: 57-58; Smedes 1996: 65-69; na Sande 2004: 20, 34.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kutatua tatizo kwa njia inayojenga. Tunapokumbuka msamaha wake na kukaribia uwezo wake, tunaona vitu kwa wazi zaidi na kwa namna tofauti na tunaitikia katika migogoro kwa hekima zaidi. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kupata suluhisho bora zaidi kwa matatizo yetu. Wakati huo huo tunaweza kuwaonyesha wengine kwa hakika yupo Mungu anayefurahia kutusaidia sisi kufanya vitu ambavyo tusingeweza kuvifanya wenyewe." (Sande 2004: 20)

**b.** *Sande anaelezea vidokezo vya kivitendo vinavyomfanya mtu aweke mtazamo wake kwa Bwana:* "Moja ya njia bora zaidi ya kuweka mtazamo wako kwa Bwana ni mara zote kujiuliza maswali haya: Nitawezaje kumheshimu na kumpendeza Mungu katika hali hii? Kipekee, kwa namna gani nitamsifu Yesu kwa kuonyesha kuwa ameniokoa na ananibadilisha? Kutafuta kumpendeza na kumheshimu Mungu ni dira yenye nguvu sana kwenye maisha, hasa wakati tunakutana na changamaoto ngumu. Yesu mwenyewe aliongozwa na malengo haya [tazama **Yoh 5:30; 8:29; 17:4**]. . . . Wakati anaweka wazi utajiri wa upendo wa Mungu na kumpendeza yeye kuwa muhimu zaidi kuliko kushikamana na mambo ya kidunia na kujipendeza mwenyewe, kuitikia kwenye migogoro kwa neema, kwa hekima na kwa kuwa na kiasi inazidi kuwa jambo la kawaida. Mtindo huu humpa Mungu utukufu na kuweka msingi wa upatanisho wenye mafanikio." (Sande 2004: 34)

**B.** ***Kusamehe ni muhimu kwa ajili ya usalama wetu wenyewe***[10]

**1.** Kusamehe mara zote ni njia pekee ya kumaliza deni. Kama Jeffress anavyofafanua, katika mfano wa Yesu, "Mtumwa alikuwa anadaiwa deni ambalo asingeweza kulilipa kwa miaka elfu. Kwa hiyo mfalme alikuwa na njia nyingine zaidi ya msamaha?" (Jeffress 2000: 51) Kumwadhibu na kumtesa mkosaji hakutasababisha *kulipwa hata senti moja* ya deni. Kwa kweli, mengi ya "madeni" tunayodai *hayana thamani:* mkosaji anaweza akawa amefariki; anaweza akawa ametoroka; anaweza asiwe anatujali hata kidogo. Zaidi, wakosaji wengi hawawezi kulipa kwa namna yoyote ile. Je ni malipo gani yangetosha kuwa fidia kwa ajili ya mtoto wako aliyeuawa na dereva aliyelewa? Au hadhi yako iliyoshushwa kwa maneno ya uongo? Au ndoa yako iliyosalitiwa kwa uzinzi? Au uaminifu wako ulioharibiwa kwa kubakwa? Ukweli ni kwamba msamaha utakuweka huru mbali na deni lisilolipika unaloshikilia.

**2.** Kusamehe hutuweka huru kutoka kwenye vifungo vya zamani na mkosaji. Kusamehe kunatuweka huru na kutufanya tuendelea na maisha yetu wenyewe. Kusamehe kunatuweka huru kutoka kwenye minyororo isiyoonekana, lakini halisi,-inayotufungu kwenye wakati uliopita—mabaya yaliyopita, maumivu, na minyororo ya uovu inayotuzuia sisi tusiishi kwa furaha, amani na kwa uhuru. **Waeb 12:1-2** inatuambia yatuapasa "weka mbali kila mzigo mzito, na ile dhambi ituzingayo kwa upesi," na "kuenenda kwa uvumilivu katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu." Kutosamehe kunatuzuia sisi kufanya hivyo, kwa sababu kutokusamehe kwenyewe ni yote mawili yaani mzigo mzito na dhambi na huweka mtazamo wetu kwenye kosa na kwenye jeraha badala ya Yesu. Kusamehe kunatuweka huru na kutuwezesha kukimbia mbio yetu bila minyororo na tukiwa tumeelekeza macho yetu kwa Yesu.

**3.** Kusamhe kunatuweka huru mbali na mateso yasiyo na sababu.

**a.** *Kutokusamehe kunaweza kukuangamiza wewe.* Kucheua ubaya uliotendewa wewe, kulea uchungu, ni kudonoa kwenye donda lililo wazi, kukataa kuliruhusu lipone. Kuendelea kwetu kucheua kukwazika, kubaki kwetu katika uchungu nafsini mwetu, mawazo yaliyojaa chuki, kutaka kwetu kulipiza kisasi, hakumwumizi kabisa kabisa mtu mwingine, na hakuletei sisi jema lolote—vinatufanya sisi tuharibikiwe tu.[11] Mawazo haya hufanya "nafsi zetu zinywee" (hivyo kunena), na kutufanya sisi tusimfananie Kristo badala ya kutupeleka karibu na Kristo. Kwa hakika, hatuwezi "kamwe kufika" hata hivyo, kutosamehe, kucheua maumivu, na kulea uchungu kwa kukataa kutii huleta matokeo mabaya zaidi kwa roho *za watu ambao walishateseka sana.* Ingawa chuki inaweza kutupa aina ya "nguvu ya ghafla," kadiri muda unavyoenda inabadilika kuwa nguvu inayopambana na mwenye chuki.

**b.** *Kutosamehe kulikodumu huambatana na matatizo ya moyo yanayoongezeka, kufanya neva za ufahamu kuwa na kasi zaidi ya kawaida, mkandamizo wa damu kuongezeka, na kuna uwezekana wa kupungukiwa na nguvu ya mwili kujikinga na magonjwa.* Kwa upande mwingine, kusamehe kunaambatana na kupungua kwa matatizo ya kisaikolojia, hupunguza

[10]Sehemu hii kwa ujumla ni kwa mujibu wa Jeffress 2000: 50-57; Smedes 1984: 125-51; na Smedes 1996: 55-74.

[11]Ni kama hayati Mwigizaji wa Kiamerika, Buddy Hackett, alivyosema, "Mimi nimekuwa na mijadala michache na watu, lakini hawana uchungu. Unajua ni kwanini? Wakati wewe una uchungu, wao wapo nje wanacheza." (Jeffress 2000: 53)

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kiwango cha hasira, kukua kwa ukomavu wa kihisia (McCullough 2000: 43-55; Witvliet, et al., 2001: 117-23; Enright 2001: 45-67).

**4.** Kutokusamehe kunadhuru mahusiano yetu na wengine. Kwa kujifanya sisi wenyewe kuwa na uchungu, watu walio na mioyo migumu, wanaojitazama wao wenyewe na ubaya tuliofanyiwa, kutosamehe kunatutenga na watu wengine.

**5.** Kutokusamehe kunaathiri mahusiano yetu na Mungu. Dhambi, pamoja na dhambi ya kutosamehe, inatutenga na Mungu (**Isaya 1:10-15**; **59:1-2**; **Mika 3:4**). Kutengana huku na Mungu kunaathiri maisha yetu katika dunia hii. Zaidi, kama anavyoeleza Carson: "Msisitizo [katika Maandiko] unaegemea kwenye faida ya milele kwa kule kuishi sawa sawa na Mungu. Na katika nuru ya baadhi ya vifungu (k.m., mfano wa mtumishi asiye mwaminifu ulionukuniliwa hapo juu), kuna hatari nyingi za binafsi na za ndani za kutokusamehe wengine. Kwa maana hakuna, hakuna kabisa kilicho muhimu zaidi kama kuhakikishiwa msamaha na Mungu." (Carson 2002: 80)

**6.** Kusamehe kunawapasa watu wenye makosa kama sisi. Watu wengi si kwamba wao tu wanakosewa sana, sisi si waathirika pekee. Lakini, sisi pia tunawakosea wengine; sisi pia tunawakwaza wengine. Katika "ulimwengi halisi" kusamehe ni njia ya maisha—unapomwumiza rafiki wa karibu kwa njia ya kumsema isivyo sahihi au kwa tendo (na sisi sote hufanya hivyo), rafiki yetu wa karibu ataumia na kuachilia. Kwa hiyo, kufuta deni na kuachilia ni njia ya maisha. Maisha yasingewezekana kama watu wasingekuwa wanasameheana kila wakati.

**7.** Kutokusamehe ni uchaguzi, kama vile ambavyo kusamehe ni uchaguzi. Tunabagua kuhusu nani tumsamehe na nini tusamehe: tunasamehe tu maumivu "kidogo" na wale waliokosewa na watu wa karibu nao. Hata hivyo, Yesu hakutupa hiari katika kuchagua maumivu, au watu, ambao tunatakiwa kuwasamehe. Alisema tunapaswa kusamehe "hata saba mara sabini" (ambayo ni lugha ya alama ya Yesu, kusema "bila mwisho" na wala siyo mara 490) (**Math 18:22**); tunatakiwa kuwapenda *adui* zetu, siyo tu wale wanaotupenda sisi (**Math 5:38-48**). Yesu ni makali sana kwa wenye dhambi (kama sisi) wanaokataa kusamehe wenye dhambi wengine, kwa sababu sisi *sote* ni wenye dhambi  Smedes, anatoa mtazamo wake katika mfano wa Yesu (**Mathayo 18**), anasema vema: "Yeye [Yesu] ni mkali kwa sababu utata wa wenye dhambi kukataa kusamehe wenye dhambi kunashangaza ufahamu wa Mungu. Hawezi kuchukuliana nayo; hakuna namna ya kiungwana ya kulichukuliana na hili. Kwa hiyo asema, kama unataka msamaha wa Mungu na wewe unashindwa kumsamehe anayehitaji msamaha kidogo, sahau kuhusu msamaha unaotaka. Ukiacha namna kiingereza cha King James kinavyosema, unapata Yesu anasema kitu kama hiki: ukikataa kusamehe watu wengine wakati wewe unategemea kusamehewa, unaweza kwenda motoni." (Smedes, 1984: 150)

## IV. Jinsi ya kusamehe[12]

### A. *Kanuni ya Kusamehe ya Worthington iliyo na UTAJIRI*

Worthington ana kanuni yenye hatua tano, ambao anaitazama kama piramidi (Worthington, 2003: 73):




**1.** Vuta hisia ya maumivu. Ili kumsamehe aliyekukosea kwanza tunatakiwa kuwa wakweli kuhusu

[12]Sehemu hii kimsingi ni kwa mujibu wa Worthington 2003: sura. 4-8; na, kwa upili, ni kwa mujibu wa Smedes 1996: sura ya 15-20; na Enright 2001: sura ya 4-12.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

maumivu na kosa lenyewe.

**a.** *Tunaweza kukana au kupunguza maumivu kwa sababu tumeumizwa sana. Au tunaweza kuitikia kwa kupitiliza kwa maumivu na makosa madogo; tunaweza kudhani mkosaji ametufanyia ubaya nkubwa zaidi kuhusu kile alichotufanyia kihalisia, au tunaweza kufikiri kitu kama, "Kama hili lisingetokea, ningekuwa na furaha zaidi, na mafanikio zaidi, tungekuwa na maisha mazuri zaidi"* (Enright 2001: 110). Tunahitaji kutathmini kwa uhalisia kabisa asili ya kosa, na madhara yake kwetu, na jinsi tulivyokuwa tukiitikia (tazama Sande 2004: 80: "Wakati unapima nafasi yako katika mgogoro, inasaidia kuona aina mbili za makosa. Kwanza, unaweza kuwa na *mtazamo wa kihisia uliopitiliza,* unakufanya ukwazwe kirahisi na tabia ya watu wengine. Pili, unaweza ukawa umechangia mgogoro kwa *tabia yako ya dhambi."*).

**b.** *Worthington anapendekeza mbinu fulani kutusaidia kutafakari maumivu.* Tunatakiwa kuanza na maombi, kuomba uwepo wa Bwana kama mlinzi wetu na kumwalika Roho Mtakatifu kama mfariji wetu. Tunapaswa kujilinda wenyewe tunapojikumbusha maumivu na undani wa mazingira yanayohusika, hakikisha hatuingii kwenye hasira, hofu au mfadhaiko. Jaribu kukumbuka nini kilitokea, lakini na vile ulivyohisi kuhusu kilichotokea; kwa usahihi toa majina kwa hisia zako, (jaribu kuwa mkweli kwa kadiri iwezekanavyo). Jitawale mwenyewe kwa kuwa mwenye furaha, mtaratibu na vuta pumzi sawa sawa. Jaribu kunona mambo kwa mtazamo wa mtu mwingine. Itasaidia kusamehe yale mambo madogo kabla hujarukia makubwa mabaya ya uhalifu ambayo wakati mwingine hufanyika. Hayo yote yanaweza kuwa yanaumiza, lakini ni hatua ya kwanza katika kuelekea kwenye uponyaji na uzima.

**c.** *"Maumivu anayotusababishia mtu mwingine yanasababisha kirahisi tujiulize swali: Utafanya nini kwa ajili yangu? Hatukutaka kupatikana na hili na tunataka kuondokana nalo. Lakini limetung'ang'ania. Yatupasa kulimiliki. Na tunaanza kumiliki maumivu yetu ikiwa tutaanza kujibu maswali yake." (Smedes 1996: 135)* Kuna uchaguzi wa aina mbili tu: "Tunaweza kujaribu kusahau, kumeza katika fahamu zetu na kuwa mzigo utakaotusumbua ndani yetu. Au tunaweza kusamehe na kuponya. . . . Tutakachochagua ni hiari yetu. . . . Tunaanza kuwajibika kwa ajili ya maumivu yetu tunaposikiliza maswali yake. Tunaanza kupona tunapotoa majibu sahihi kwa maswali yake." (Ibid.)

**2.** Hurumia. Kumhurumia mkosaji ni kuelewa utu wake, n/y., alichokuwa anawaza, matokeo ya tukio kwake mwenyewe. Kuhurumia ni kuona kwa hakika kwamba, ikiwa kama wewe ndiyo umevaa viatu vyake, wewe mwenyewe pengine ungefanya sawa sawa kama alivyofanya. Kuhurumia ni kuanza kumwona yeye kama Mungu anavyomwona: kama mwanadamu (sawa sawa na wewe mwenyewe) na si kama "kitu". Hii inawezekana ni sehemu ngumu kabisa ya kuweza kusamehe "Msamaha wa kihisia." Sisi hatuwezi kwa nguvu zetu wenyewe, kuwapenda adui zetu. Katika nguvu zetu wenyewe mara zote tunataka tuwaumize adui zetu, tunataka kuona wakilipa kwa walichofanyia, kuona wanaumia kama sisi tulivyoumia. Tunataka kushusha moto kutoka mbinguni uje juu yao. Na bado Yesu anasema tuite Baraka kutoka mbinguni ije juu ya adui zetu. Hatuwezi kupenda adui zetu kwa nguvu kama Yesu anavyoagiza sisi tuwapende—ni kwa msaada wa Mungu tu. Hata kama hatutavaa viatu vyao, tunaweza kujifunza njia za kuwa na huruma, na kuonyesha huruma kwa wale waliotuumiza sisi—na hatimaye kuwapenda adui zetu. Msamaha wa kweli, unaodumu na unaobadilisha maisha inategemea kule kuhisi tofauti kuhusu mtu aliyekuumiza.

**a.** *Kati ya 1985-1995 Worthington na wenzake walijifunza na kulinganisha aina nbili za msamaha kutoka kwa zaidi ya wanandoa 1000 au watu binafsi: msamaha unaomfaidisha mtu binafsi (i.e., "kusamehe ili kupata"—kusamehe ili kujisikia vizuri, ili kuweza kuendelea na maisha n.k.) na msamaha wenye msingi katika huruma(i.e "kusamehe ili kutoa"—kusamehe kwa sababu wewe, mwathirika unacho cha kutoa ambacho mkosaji anahitaji: msamaha).* Matokeo aliyopata ni ya kushangaza: "Watu wanaosamehe ili kupata faida wanasamehe haraka sana kuliko kundi lile linalosamehe ili kuhurumia. . . . Saa moja au masaa nane—ya msamaha kwa ajili ya faida ya anayesamehe yalitosha kabisa. Kwa wale wanaosamehe kwa ajili ya faida ya mtu mwingine, saa moja inasababisha msamaha kidogo sana. Masaa nane yalitoa msamaha mkubwa sana—zaidi ya mara tano ya msamaha wa saa moja na mara tatu ya ule unaolenga kujipatia faida binafsi.

Zaidi ya hayo, tulipotazama pamoja na watu wiki sita baadaye, kiwango cha msamaha kwa kundi linalosamhe kwa ajili ya faida binafsi kimeshuka kwa nusu ya kiwango kilichotolewa mwishoni mwa matibabu. "Kile kikundi kinachosamehe kwa kuhurumia, kiwango cha msamaha kilibakia juu hata baada ya matibabu kuisha." (Worthington, 2001: 13-14) Worthington anahitimisha: "Msamaha hautufaidishi sisi. Lakini ikiwa tutasamehe ili kupata,

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

tunapata kidogo tu ya kile tunachotarajia. Lakini tukisamehe tukilenga zaidi kupata, tunapata tone tu ya faida. Ikiwa tutatoa zawadi ya msamaha kwa muhitaji mkosaji, ingawa, tunapokea uhuru, amani, na pengine afya na kurejea kwa mahusiano. Msamaha hutoka kama maji kutoka kwenye bomba. Unatusafisha. Unatuweka huru." (Ibid.: 14)

**b.** *Huruma hujitokeza katika hatua tatu:* (1) Uelewa (i.e., unaelewa jinsi mtu mwingine anavyoona mambo); (2) Kujilinganisha kihisia (i.e., unahisi na kufikiri *pamoja* na mtu mwingine); na (3) Huruma (unahisi kuwa na huruma *kwa ajili* ya mtu mwingine, vile vile na kumwelewa na kuwa na hisia sawa na yeye). Kupata msamaha wa kina, unaodumu, unahitaji kufikia kina kirefu kuhurumia, kuhurumia kwa rehema.

**c.** *Kuzingatia kweli kadhaa kutaongeza uelewa wetu wa, huruma yetu kwa ajili ya, mtu mwingine:* (1) "Hisia laini" (k.m., hofu, msongo, woga, na maumivu) mara nyingi hasira ya ndani, ukatili, na kushambuliwa na mtu; (2) Watu wanashawishiwa na mazingira yao, hali na nafasi; (3) Watu "wameunganishwa kwa nguvu" na usalama wao (na kwa hiyo huitikia ghafla katika mambo yanayoonekana kama matishio kwao); (4) Watu wameathiriwa na uzoefu wa siku zilizopita (wanaweza kuitikia kwa hofu na hasira sasa kwa sababu ya jinsi walivyokuzwa, au uzoefu mwingine walioupitia zamani huko nyuma); (5) Watu mara nyingi huitikia kwenye mambo bila kufikiria (hii ni kweli hasa wakati watu kihalisi, wanaitikia kutokana na kuumizwa, kwa haki au kwa ubaya, na hali hiyo ikawa ni tishio kwao); (6) Tusisahau kamwe kwamba *sisi ni wakristo* (na, kwa hiyo, kwa neema ya Mungu, na kutumia nguvu za Roho Mtakatifu, tutaitikia kwa tendo au maumivu tuliyopata kutoka kwa mtu mwingine tukiweka mbali utu wetu wa kale, tukiwa wakweli na wenye upendo na kuvaa "nia ya Kristo" ambaye sisi kwa hakika tunayo nia yake (tazama **Waef 4:15, 20-32**; **1 Wakor 2:16**).

**d.** *Mbinu mbalimbali zinaweza kutusaidia kumhurumia mtu mwingine:* (1) Omba kwa ajili ya karama ya huruma; (2) Andika barua inayoeleza kana kwamba wewe ndiye Yule mtu aliyekuumiza wewe, ukielezea misukumo ya mkosaji, mawazo na hisia alizonazo yeye; (3) Andika barua ya kuomba msamaha kwa mtazamo wa mkosaji; (4) Ongea na kiti kitupu, ukimwambia mkosaji unachofikiri na kuhisi, kana kwamba mkosaji ameketi kihalisia katika kiti hicho-halafu fanya kinyume chake, kwa kukaa kwenye hicho kiti na kujiona kana kwamba wewe ndiyo mkosaji, ukimweleza kile kilichokusukuma ufanye yale uliyofanya, na kuomba msamaha kwa yale uliyofanya; (5) Ongea na rafiki au shiriki katika kikundi cha waumini wenzako kusaidiana kuhusu mambo ya msamaha; (6) Fanya au tengeneza kitu fulani kuashiria hisia zako za huruma kwa mtu mwingine; (7) Tafakari juu ya huruma za Yesu kwa watu kama mtu huyo; (8) Omba kwa ajili ya huyo mtu mwingine [siyo moto wa mbinguni umwangamize, lakini Mungu amkaribie, na kumbariki, na amgeuze na kumfanania Kristo, hata hivyo wakati wewe unaomba hivyo hayo hayo yanatokea kwako]; (9) Tafakari kuhusu makosa yako mwenyewe, udhaifu, jinsi ulivyoumiza, ulivyolaghai, ulivyotumia, ulivyodharau, upuuzaji, na vinginevyo ulivyokwaza wengine.

**3.** Zawadi ya Msamaha isiyo na ubinafsi. Tafiti zinaonyesha ikiwa watu hawana rehema, kwa hakika hawataweza kusamehe. Pamoja na hayo, hata baadhi ya wale wanaojenga huruma kwa ajili ya mkosaji hawasamehi.

**a.** *Wakristo wanahitajika kutafakari dhambi zao wenyewe zilizosamehewa na Mungu na watu wengine waliowasamehe.* Ili kupata uelewa wa kina wa ubinadamu wetu wenyewe na unyenyekevu inafanya iwe rahisi kusamehe wengine waliotukosea. Kwanza kukumbuka makosa yetu, kisha tutakumbuka uhuru wa kina na shukrani tulizokuwa nazo tuliposamehewa mokosa yale. Shukrani na unyenyekevu ni matendo ya msingi ya ukristo yanayotufanya sisi kuangalia mambo ya wengine.

**b.** *Kutokuwa mbinafsi ni upendo unawaelekea wengine; ni kutoa bila kutegemea kupata kitu. Moja ya zawadi kubwa tunazopokea ni zawadi ya kusamehewa—ni kuweka huru; ni kuinua; inweza kuwa inabadilisha maisha.* Ni zawadi ambayo Kristo ametupa sisi na ambayo watu wengine wametupa sisi. Msamaha ni "nguvu kamilifu" ya *upendo*. Hivyo, ingawa chuki inaweza ikatupa sisi "nguvu ya kitambo ya kuendeleza ukatili kwa siku ya leo . . . chuki haina nguvu ya kudumu ya kuandaa hatima nzuri zaidi ya kulipa kisasi. Ni msamaha ndiyo unaotoa chemichemi ya uponyaji ya kudumu kwa siku zijazo. Kwa mwendo mrefu msamaha una nguvu kuliko chuki." (Smedes 1984: 146) Mkristo mwenye kina ni mtu mwenye shukrani yenye kina; mtu mwenye shukrani hawezi kusaidia bali zawadi ya msamaha ambayo imempatia faida kubwa.

**4.** Toa msamaha hadharani. Unasamehe, kwanza na kwa umuhimu mkubwa, ndani yako mwenyewe—

moyoni mwako, katika ufahamu wako, na nafsini mwako; na kujitoa hadharani kusamehe baada ya kuwa angalau umetoa "msamaha wa maamuzi," kama siyo "msamaha wa hisia," ndani ya moyo wako mwenyewe na ufahamu.

**a.** *Kujitoa hadharani kwa uamuzi ambao umefanya kibinafsi inasaidia kukazia uamauzi ule na kushinda mashaka juu ya ama "umemsamehe sawa sawa" mkosaji, ambayo yanaweza kutokea nafsini hapo baadaye, wakati unaporejea kufikiria juu ya mkosaji au tukio.* Kujitoa kusamehe hadharani, ni kama, kubatizwa au kushiriki meza ya Bwana—"ni ishara inayoonekana kwa nje ya neema ya kiroho iliyomo ndani" ya msamaha uliokwisha kuutoa.

**b.** *Kuna mbinu kadhaa ya kujitoa hadharani kusamehe:* (1) Tiisha ufahamu wako kutomdhalilisha mwenzako pale mawazo hasi yanapotokea (jiambie mwenyewe "achilia" ku-"acha kutafuta kosa"; "badili maudhui katika ufahamu" wakati mawazo hasi yanapojiingiza). Vivyo hivyo, tafakari juu ya, rudia, hata andika, mambo *chanya* ya huyo mtu mwingine. (2) Weka ishara ya msamaha wako. Andika kosa kwenye mkono wako; kwa kuosha mara kwa mara na kazi itafutika. Au, beba jiwe kubwa kwenye mkono wako ulionyoosha (kama lile "jiwe la kwanza" ambalo Yesu alitoa mwaliko litupwe kwa mwanamke kahaba aliyefumaniwa [**Yoh 8:7**]); ona msongo na maumivu unayopata kama maumivu na msongo wa kutokusamhe—wakati uzito wa ile shauku ya kulipa unapokuwa mkubwa kiasi kwamba hutaki kuendelea kushikilia tena zaidi, achilia jiwe lianguke kutoka mkononi mwako kama ishara ya kusamehe kwako. Au, andika kosa kwenye karatasi, na kisha choma kwa moto na sambaza majivu. Au, andika kosa kwenye karatasi na upigilie kwa misumari kwenye msalaba wa mti, au iache kwenye au chini ya msalaba kanisani kwako. Kwa kuyafanya haya yote, kumbuka kwamba pia unatoa kutokusamehe kwako, na maumivu yako, kwa Yesu—yeye anajua anayabeba; huhitaji wewe kuyachukua. (3) Andika kusamehe kwako. Andika rasmi "cheti cha msamaha" ambayo utatunza ili kukuhakikishia nyakati za mashaka kwamba kwa hakika, ulishamsamehe kikamilifu aliyekukosea. (4) Mwambie mtu mwingine kuhusu kusamehe kwako. Mwambie Mungu, wewe mwenyewe, mwenzi wako, rafiki unayemwamini, mchungaji wako, watu hawa wote watakusaidia nyakati za mashaka. (5) Mtendee mtu mwingine kana kwamba umeshamsamehe. Kadiri tabia yako inavyokuwa njema, itakazia uamuzi wako wa kusamehe uliochukua na hisia zako za huruma na upendo.

**5.** Tunza msamaha. Mawazo na hisia za kutosamhe zinaweza kuinuka ndani yetu (kama vile ambavyo mawazo ya dhambi—tamaa, ulafi, kiburi, chuki, n.k.—vinavyoweza kuinuka ndani yetu). Kwa kumwona Yule mtu, akiwa mahali fulani maalumu, kwa kusikia jambo fulani, tarehe ya maadhimisho, na mambo mengine, au tunapokuwa tumechoka, wapweke, au tunapokuwa na msongo, yaweza kusababisha mawazo na hisia zisizotakiwa za kutokusamehe kuinuka ndani yetu. Ni katika nyakati kama hizi tunatakiwa kushikilia msamaha wetu *ambao tulikwisha toa* na ambao *tuliutoa hadharani.*

**a.** *Kuna mbinu kadhaa zinazoweza kutusaidia kushikilia msamaha katika nyakati hizo:* (1) Tambua kwamba maumivu ya jeraha la kukumbuka siyo sawa na yale ya kutosamehe (kutosamehe kunahitaji kucheua; usijiachilia kucheua kunakokusudia kulipa kisasi); (2) Usiishi kwenye hisia hasi (Kwa kujishughulisha jitoe mwenyewe—imba, omba, msifu Bwana, fanya kazi fulani ya kushughulisha viungo—kuliko kukaa katika mawazo au hisia zilizojaa maumivu na chuki); (3) Jikumbushe mwenyewe kwamba ulishamsamehe yule mtu (na jikumbushe zile nyakati ulipojitoa mwenyewe hadharani kusamehe); (4) Tafuta kujihakikishia kutoka kwa mwenzi, mshirika au rafiki (mtu fulani uliyemshirikisha kusamehe kwako aweze kukusaidia katika nyakati za mashaka au msongo); (5) Tumia kumbukumbu ulizoweka (soma "cheti cha msamaha," barua, au maandishi mengine uliyoandika yanayoweka kumbukumbu ya kusamehe kwako); (6) Tazama tena, pitia kwa upya katika mawazo, na tendea kazi tena mtindo wa utoaji wa msamaha.

**b.** *Fanyika mtu wa kusamehe zaidi*. Hii huchukua maisha yote, lakini inasaidia kukuumba na kumfanania zaidi Kristo. Zaidi, kanuni ya kufanyika kuwa mtu wa msamaha zaidi inakusaidia wewe kufanya "halisi," na kushikilia, msamaha uliotoa kwa mtu fulani kutokana na kosa fulani maalumu. *Kuna kanuni kadhaa zitakazokusaidia kufanyika kuwa mtu wa msamaha zaidi:* (1) Fikiria kwa nini unataka kuwa mtu wa kusamehe zaidi Mwombe Bwana auchunguze moyo wako: je misukumo yako ni ya kibinafsi, au kwa sababu unataka kuwa mtii na mwenye kiasi, au una misingi ya shukrani, upendo na huruma? (2) Tambua majeraha yako makubwa ya huko nyuma na samehe. Kadiri unavyoweza kusamehe makosa ya huko nyuma na kujifunza katika hayo, ndivyo inavyozidi kuwa rahisi kwako kusamehe majeraha yatakayojitokeza siku zijazo. (3) Samehe jeraha moja kwa wakati mmoja. Kazana kutoa msamaha wa kimaamuzi na wa

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kihisia; kadiri unavyoendelea na muundo wa REACH, chunguza maendeleo yako ili kuonyesha kwamba kuna maendeleo. (4) Tambua mashujaa wa msamaha. Kusoma kuhusu, au kuongea kuhusu, watu waliosamehe sana inaweza kuwa na uvuvio zaidi na kututia moyo. (5) Jipime mwenyewe. Kutokusamehe kunaweza kukawa tabia mbaya, kwa hiyo kuwa mwungwana kwako mwenyewe na tunza "wajibu wa kusamehe." (6) Punguza sifa mbaya na palilia haki. Kwa kudhamiria kazana kuwa na haki zaidi ya kusamehe tu. *Jielekeze kipekee* si juu ya nini cha *kuepukwa* kufanya tu bali lipi *utafanya* ili kuwa mtu mwenye haki zaidi. Kwa mfano, amua ni tabia ipi utahitaji kujenga na kisha andika utakachofanya kudhihirisha tabia hiyo: k.m., "Kama ningekuwa na (upendo) zaidi ninge (*tia moyo watu, ningejaribu kuwaelewa zaidi, kuwasikiliza*) mara kwa mara." (7) Badilisha uzoefu wako uliopita. Tumia huruma yako na waza kwamba Yesu anamtia moyo mtu aliyekuumiza. Hii itasaidia kudhania kwako na kumbukumbu zako za maumivu ya tukio lililopita. (8) Weka mpango mkakati wa kujiendeleza mwenyewe Jaribu kukabili maisha yako kwa kudhamiria na kidhamira, ukijipa muda wa kutafakari na kuomba, kupanga na kupumzika.. Maisha yaliyolemewa na shughuli ni magumu sana kuyatiisha, matokeo yake, msamaha wetu, huruma na upendo kwa wengine huwa vigumu. (9) Fanya mazoezi ya kusamehe katika mazingira ya kinadharia. Kufanyia mazoezi msamaha kabla kuhusu hali zinazoweza kujitokeza inaweza kukusaidia pale mazingira halisi yanayohitaji msamaha yanapojitokeza. (10) Fanyia mazoezi msamaha siku kwa siku. Unapopanga shughuli zako za siku, fikiria kuhusu watu utakaoshughulika nao siku hiyo. Waweke kwenye maombi, na hali za kuumiza zinapotokea tumia ule mtindo wa kusamehe vilivyo. (11) Tafuta msaada kwa mtu. Rafiki unaowaamini, wachungaji, na wengine waliofunzwa na wenye uzoefu katika maandiko na katika stadi za kusamehe wanaweza kutoa ushauri wa kufaa na msaada. (12) Anza kampeni ya kuwapenda adui zako. Au kibinafsi, au ni vizuri zaidi, ukiwa na kundi unalohusiana nalo kanisani, omba, panga, na fanyia kazi mikakati kwa *kufanya mema* kihalisi kwa adui zako. Uwe na juhudi katika kuonyesha upendo wa Kristo kwa wale wasiopendeka.

**B.** ***Kumwambia mkosaji "Nimekusamehe"***

**1.** Kihalisia kumwambia mkosaji "Nimekusamhe" kunatakiwa kufanyike kwa uangalifu: siyo mara zote ni sahihi au muhimu. Kufanya hivyo kunaweza kutumika kama silaha dhidi ya mkosaji, au inaweza kufanyika mapema zaidi, kumfanya mkosaji kuitikia kwa kujitetea na kuongeza majeraha mapya kwenye yale ya zamani. Zaidi, unatakiwa kuwa makini pale unapoenda kueleza msamaha wako, unaweza ukajiweka wazi kwenye hatari ya kushambuliwa kimwili au ugomvi kutoka kwa huyo mtu.

**2.** Smedes anashauri kwamba, kabla ya kusamehe, unapaswa: a. *Kufikiri* (fahamu vema kwa kadiri uwezayo kuhusu kilichotokea); b. *Tathmini hali ilivyokuwa;* c. *Ongea na rafiki au mshauri;* d. *Hisi* (elewa hasa unachohisi na kwa nini); na e. *Omba* (kusamehe ni tendo la mguso ili kutenda—tunatakiwa kuwa wakweli kwa Mungu, eleza hitaji letu kwa ajili ya msaada wake, uombe, na utumie unapokufikia). Kisha, wakati umeamua kihalisia kumwambia mtu mwingine kwamba umemsamehe, unapaswa: a. *Tumia muda wako;* b. *Tambua madhara yatakayotokea;* c. *Ngojea ishara;* d. *Fanya kwa kuzunguka* (ongea kwanza kuhusu mambo mengine; sikiliza kwa muda; fanya kama wazo lililokuja wakati huo); e. *Fanya baada ya kuanza mazungumzo kiungwana na kwa ushawishi, ukimtakia mema mwenzako;* f. *Usidai kuona hali ya msukumo wa utakatifu;* g. *Chukuliana;* h. *Fanya fupi;* i. *Fanya nyepesi;* na j. *Mpe mtu mwingine wakati* (badili mada kama hayupo tayari kuliongelea; mruhusu alifikirie; mwache aendelee na vile alivyokuwa). (Smedes 1984: 138-39, 145-46)

**3.** Hali zinazofaa sana kiuhalisia za kusema maneno ya msamaha kwa mtu mwingine yanaangukia katika mazingira yafuatayo:[13]

**a.** *Mkosaji anapokuwa amekiri na ameomba msamaha.* Mkosaji anaweza kuwa tayari kusikia maneno hayo ya muhimu sana kabla hujawa tayari kuyatoa. Kumbuka msamaha hauwezi kulazimishwa—ni tendo lako la hiari. Mwitikio wako wa kiungwana unaweza kuwa, "Ninataka kukusamehe, lakini nipe muda kidogo, SAWA?"

**b.** *Mkosaji kamwe hajakiri kosa wala hajaomba msamaha, lakini hatia imejengwa pasipo shaka yoyote.* Unaweza kutoa msamaha kwa mkosaji ukitumaini kwamba ataomba msamaha (ambao ameung'ang'ania kwa sababu ya aibu) baada ya kupokea msamaha wako; hata hivyo atakapobakia hali ya kutotubu, bado unaweza kuondokana na hali hiyo ukijua kwamba umefanya kila linalowezekana.

[13] Hiki kisehemu kimsingi ni kwa mujibu wa Enright 2001: sura ya 11.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**c.** *Mahusiano kati yako na mkosaji yamevunjika na pande zote mbili zina hasira.* Upande *usio na hatia* unaweza ukaanzisha mchakato wa upatanisho kwa kuomba *msamaha* kwanza, ambao unaweza ukasababisha upande wa pili kuelezea masikitiko yake, ambayo yatafungua mlango kwa wewe kutoa msamaha.
**d.** *Kosa lilifanyika muda mrefu uliopita, na mkosaji si sehemu tena ya maisha yako.* Fursa inaweza isitokee ya kueleza msamaha kama huyo mtu amekufa, au hapatikani tena kwa sababu zingine. Hata hivyo, unaweza ukaonyesha kusamehe kwako kwa ishara (kama ilivyoelezwa hapo mapema), au ukaelezea msamaha wako kwa mwanafamilia ya mkosaji, ukoo, kabila au kanisa au watu wengine wa kati ili kufanya kikao cha kusameheana.
**e.** *Mkosaji hana wazo kwamba wewe umekwazika.* Mtu anatakiwa alete hoja hiyo ya zamani kiufundi sana; kama ilivyodokezwa mapema, unatakiwa kuzingatia kwamba inawezekana kuanzisha mjadala wa jambo unaweza kuleta madhara zaidi au mema zaidi kwa mtu mwingine vile vile na kwako mwenyewe.

**C.** ***Miongozo mingine kwenye njia ya msamaha***

**1.** Samehe *bure,* au kihalisia huta "samehe" kabisa. Huwezi "kufanywa" au "kulazimishwa" usamehe.
**2.** Msamaha ni *uchaguzi*; msamaha unakuhusisha *wewe mzimamzima*; msamaha ni *mchakato:* msamaha huchukua *muda* (yawezekana maisha yote); msamaha unahitaji kufanyiwa *kazi* (unaweza kutumia juhudi kubwa kwa kipindi kirefu); msamaha ni *badiliko* (*wewe* utabadilika; njiani wewe utaona, Kristo ataona, na wengine wataona, ni kwa kiasi gani umeendelea kumfanania Kristo kama matokeo ya kazi ya kusamehe, mara nyingi inayochukua muda mrefu, ngumu, na ya polepole). Kwa hakika, Klassen anaenda mbali zaidi akisema hili: "Kwa namna ya kushangaza, jeraha zisizosameheka zinakupatia wewe fursa adimu katika maisha: *kubadilika kimsingi.* Uzoefu wa kujeruhiwa unaweza kukulazimisha kinyume na matakwa yako kubadilisha ndoto zako, desturi zako na matarajio yako. Pengine zaidi, katika hii huzuni kubwa, lakini, twaweza kukutana na mgogoro wa msingi mara chache sana. Kuweza kujaribu misingi ya imani ya mtu ni fursa ya maisha yote. Kuifanya vizuri ni stadi. . . .

Ni katika mchakato wa kusamehe mtu mpya hujitokeza. Wakati watu wengine wasingependa kwao wenyewe na kama wangepewa uchaguzi, wangesema, 'Sihitaji kujua zaidi.' Ukweli ni kwamba siyo uchaguzi, hatujapewa kuchagua. Ni njia ya kupewa fursa nyingine, nafasi nyingine. Kuumizwa, vibaya sana, ni hali ya kufanyiwa ukarimu." (Klassen n.d.: "Kuirejesha nafsi yako")
**3.** Unaweza kutegemea kuchanganyikiwa; unaweza kutegemea kubakiwa na hasira; unaweza kutegemea kutoelewa kikamilifu kinachoendelea; na unaweza kutegemea kukwamishwa njiani. Kusamehe kunaweza kufananishwa na mtoto anayejifunza kutembea. Mtoto kwanza huchukua hatua za mtoto mdogo. Huanguka chini. Hapendi kutembea lakini anapenda kubebwa na mama yake. Pamoja na hayo, baada ya muda anapiga hatua kubwa zaidi. Anapata kujiamini na hatimaye anaweza kukimbia. Yupo *huru.*
**4.** Uwezo wa kusamehe unaweza kusaidiwa kwa kufahamu kwa uhakika kwamba *kuumia hakuepukiki.* Maumivu, majeraha, makwazo, na makosa, baadhi madogo, baadhi makubwa, ni vitu vinavyotarajiwa daima. Wanadamu ni wabinafsi. Wengi wanajali kuhusu wengine lakini hujiangalia wao wenyewe kwanza na wanafurahia kufanikiwa kwa maisha yao wenyewe. Kama ukijua hilo kwa usahihi, itakuwa rahisi kukubaliana na makosa ya watu weengine na makwazo pamoja na yako. Kama Klassen anavyoeleza: "[Kuumizwa] ni kama sehemu nyingine ya maisha, kama upendo, kazi na burudani. Baadhi ya maumivu unaweza kuyadhibiti, na baadhi yapo juu ya uwezo wetu. Mara mtu anapotambua kwamba maumivu hutokea na mengi hayawezi kuzuiwa, ndipo inakuwa ni muhimu kwamba msamaha ujengwe tu na kuwa sehemu ya maisha; na hakuna tena lisiloweza kusameheka." (Klassen n.d.: "Kanuni ya Msamaha: *Majeraha hutokea"*)

## V. Kujisamehe Mwenyewe[14]

**A.** ***Inawezekana kujisamehe mwenyewe***

**1.** Smedes husema, "Inaonekana kwangu kwamba watu wawili tu wana mamlaka ya kutoa hati ya msamaha. Mmoja ni yule tuliyemkosea. Mwingine ni Mungu ambaye anahuzunika tunapojeruhi watoto wake." (Smedes 1996: 96-97) Anaongeza, "Mtu anapoomba tumsamehe, yeye pia anaomba ruhusa ya

[14]Hiki kisehemu ni kwa mujibu wa Worthington 2003: 222-25; Smedes 1984: sura ya 8; Smedes 1996: sura ya 12; na Jeffress 2000: 183-84.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kujisamehe mwenyewe" (Ibid.: 97).

**2.** Ikiwa mtu uliyemkosea amekusamehe, kwa nini usijisamehe mwenyewe? Ikiwa umeshafanya kila unachotakiwa kufanya ili kuomba msamaha, umefanya malipizi, jutia, na umeomba msamaha, lakini mtu mwingine anakataa kukusamehe, uwezo wako wa kujisamehe kutategemea msamaha wa Mungu juu yako, na siyo dhambi kutokusamehe ya mtu mwingine.

**3.** Kama Mugu amekusamehe, wewe ni nani hata usijisamehe kwa mabaya, dhambi, na uhalifu uliofanya—na kwa majeraha na maumivu ya moyoni uliyowasababishia wengine na wewe mwenyewe? Ikiwa *huta*jisamehe mwenyewe, unajiweka mwenyewe *juu ya Mungu*, aliyekusamehe wewe. Ikiwa kuna lingine, hili linasababisha dhambi ya kiburi.

**B.** ***Ingawa kujisamehe mwenyewe inawezekana ni vigumu zaidi kuliko kusamehe wengine ni lazima kujisamehe mwenyewe inapohitajika kufanya hivyo***

**1.** Kimsingi, Yule aliyekosewa ndiyo pekee kwenye mamlaka ya kusamehe aliyemkosea: "kujisamehe mwenyewe" kunakuweka wewe katika majukumu mawili kwa wakati mmoja. Pamoja na hayo, mara kwa mara tunajiweka juu zaidi kwa sababu hiyo hiyo: tunajicheka wenyewe; tunajidanganya wenyewe; tunajipongeza wenyewe; tunajiumiza wenyewe; tunajilaumu wenyewe. Kwa nini pia tusijisamehe wenyewe?

**2.** Tunaweza kujisamehe wenyewe kwa njia ile ile tunayotumia kuwasamehe wengine. Tunahitaji kuwa wakweli kuhusu sisi wenyewe, kufahamu kosa tulilofanya, kuungama na kutubu dhambi (kugeuka kutoka) katika njia zetu mbaya. Kwa hiyo, kujisamehe mwenyewe kwa namna Fulani ni tofauti na kusamehe wengine bure hata wale waliotukosea waliokataa kutubu; kujisamehe wenyewe ni zaidi Mungu kutusamehe sisi—kama vile Mungu anavyotusamehe sisi ni kwa ajili kurejesha mahusiano sahihi kati yetu na Mungu, kwa hiyo msamaha wetu wenyewe ni kwa ajili ya kurejesha utimilifu wetu ("mahusiano sahihi na sisi wenyewe"). Kwa hiyo, toba na kujutia ni muhimu katika kujisamehe wenyewe.

**3.** Kama ilivyo aina nyingine ya msamaha, tunajisamehe wenyewe kwa mabaya matendo tuliyofanya, matendo ambayo kwayo tunajilaumu wenyewe na ambayo kwayo tunastahili lawama, na siyo kwa sababu ya sisi ni nani na vile "tulivyo." Tunaweza kufuata mchakato ambao tulitumia kusamehe wengine ili kujisamehe wenyewe. Zaidi, hakuna kuchelewa katika kujiambia mwenyewe "Mungu amekusamehe wewe na hivyo nitajisamehe." Tunaweza kurudia hayo kwa ajili yetu wenyewe wakati wa mashaka yanapotokea. Tunaweza kuwahusisha wenzi wetu, wachungaji, au marafiki waaminifu ili watusaidie katika kujisamehe wenyewe. Tunaweza kuigiza sehemu ya mtu aliyesamehewa, na kuacha kujipiga wenyewe vichwani kwa jambo ambalo Mungu mwenyewe ametusamehe ambalo kwa hilo tumefanya kila lililo katika uwezo wetu kujirekebisha na kutafuta msamaha kwa mtu tuliyemkosea.

**4.** Kujisamehe mwenyewe kunaweza kuwa na faida ya ziada ya kutupa sisi picha ya wazi zaidi ya asili yetu ya kweli tofauti na Kristo. Mara zote tunaona ugumu kukiri kwamba tumefanya mabaya—wakati mwingine kosa kubwa la kimaadili. Tunajidanganya wenyewe kwa kuamini kwamba sisi siyo kama "watu wabaya" wanaoweza kudanganya, kusema uongo, kuiba, kubaka, kuua, au kufanya aina zote za uovu. Tunapaswa kujua zaidi (tazama **Math 5:21-32**; **Marko 7:14-23**). Kukabiliana moja kwa moja na uovu mioyoni mwetu kunatusaidia sisi kupata ukweli sahihi kuhusu sisi wenyewe, inasaidia kuondoa kiburi chetu, na hutusaidia kuwa kwenye njia ya unyenyekevu. Kama vile ambavyo kusamehe wengine kunaweza kuonekana kama "ishara ya nje na alama inayoonekena" ya ndani ya msamaha wa kiroho ule ambao Kristo ametupa sisi, kwa hiyo kujisamehe wenyewe inaweza kusaidia msamaha wa Kristo kuwa "halisi" kibinafsi na katika hisia.

## VI. Toba na Msamaha[15]

**A.** ***Toba siku zote inahusika na mkosaji (yule anayepokea msamaha) siyo na mwathirika (yule anayetoa msamaha)***

**1.** "Toba" haihusishi siyo tu hisia za majuto kwa kosa lililofanyika lakini ni "badiliko la ufahamu" au "kugeuka." Kwa maneno mengine, toba ni kugeuka kutoka kwenye mwelekeo mbaya ili kufuata njia sahihi (Zodhiates, ed., 1993: *metanoéō; metánoia*).

**2.** Na katika hatua yake kina sana, toba "maana yake ni kujuta kwa kumaanisha juu ya ukweli kwamba ulichofanya ni kibaya kimaadili, bila kujali kwamba ni lazima au si lazima upate matokeo yasiyo

[15]Sehemu hii kwa ujumla ni kwa mujibu wa Jeffress 2000: ch. 4; Worthington 2003: 51-52; Smedes 1996:sura ya 11; na Smedes 1984: sura ya 7.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mazuri. Inahusisha badiliko la moyoni—*linalowezekana tu ukijua dhambi ni chukizo binafsi dhidi ya Mungu mwenyewe.* (**2 Mambo ya Nyakati 6:37-39**; cf. **Yeremia 31:19**). "Huzuni ya kimungu siku zote haiambatani ni hisia nzito, lakini inakuja na badiliko la fikra, ambalo ni lazima linalojiekeze kwenye mabadiliko ya tabia" (Sande 2004: 118-19, msisitizo ulioongezwa)

**3.** Toba inahusisha hatua nne, na "ni lazima tupite katika hatua zote nne kabla hatujamaliza" (Smedes 1984: sura.7). Hatua hizo nne ni kama zifuatazo:

**a.** *Utambuzi*: Ni lazima wewe kwanza uone matendo yako kwa macho ya mtu mwingine. Unatambua hisia hizo juu ya kile ulichofanya ni kweli.

**b.** *Hisia:* Unatoka kutoka kwenye utambuzi hadi maumivu. Unahisi maumivu uliyosababisha kwa mtu mwingine zaidi. Unashirikisha maumivu uliyoyasababisha.

**c.** *Ukiri:*

(1) Ukiri siyo tu kukiri makosa kwamba ulifanya jambo hilo lakini ni kuumia *pamoja* na mwingine, na kujiweka mwenyewe bila msaada katika mikono ya mtu mwingine. Unamwambia mtu uliyemwumiza kwamba ulichofanya lilikuwa halivumiliki na kwamba umeshiriki maumivu yao.

(2) Mahali ambapo inawezekana kufanya hivyo unatakiwa kufanya malipizi kudhihirisha kweli ya ukiri wa wako. Mfano mzuri ni Zakayo; ambaye alisema kwa ghafla na kwa hiari alisema, "nusu ya mali zangu ninawapa maskini, na kama nimemdhulumu mtu kitu, nitalipa mara nne zaidi" (**Luka 19:1-10**) (tazama Sande 2004: Nyongeza C, "Kanuni ya Fidia").

**d.** *Ahadi:* Kama toba ikiwa ya kweli, ni lazima itahitimisha kwa shauku ya wivu isiyotaka kuumiza tena na kusudio la kufanya hivyo.

**4.** Toba ni muhimu katika maeneo manne:

**a.** *Toba ni muhimu katika kupokea msamaha wa Mungu.* Tumeokolewa kwa *neema* ya Mungu tu. Hata hivyo, toba yetu ni *mkondo* ambayo kwa huo neema ya Mungu inapokelewa. Kuna tofauti kati ya *msamaha wa kiungu* na *msamaha wa mtu kwa mtu.* Tofauti hii inaonekana kati ya mtu na Mungu, ambayo inaonekana katika tofauti ya mahitaji ya Kimaandiko kati ya kusamehewa na Mungu na kusameheana sisi kwa sisi. Worthington husema: "Watu siyo Mungu. Mungu anajua misukumo ya watu; wanadamu hawawezi. Mungu anaweza kutazama ndani ya mioyo yetu na inahitaji toba. Siwezi kutazama ndani ya mtu mwingine na kujua misukumo yake. (Siwezi hata kujua misukumo yangu mwenyewe.) Hivyo msamaha wa mtu kwa mtu, katika Maandiko yote, hauhitaji msamaha wa mkosaji. . . . Katika Maandiko tunaona mgawanyo kati ya msamaha wa mtu na msamaha wa kiungu. Fred DiBlasio . . . aliorodhesha Maandiko ya msamaha wa Mungu na watu. Wengi wanaoshughulika na msamaha wa kiungu hufanya kusamehewa na Mungu kuwa ni lazima kunapokuwepo na toba. . . . Agano jipya limejaa nukuu ya maandiko ya msamaha wa mtu kwa mtu. Msamaha huo, kutokana na mistari hiyo iliyoorodheshwa na DiBlasio, ina misingi katika unyenyekevu. Wanadamu hawawezi kujua misukumo ya moyo wa mkosaji. Inabidi kwamba mwathirika alazimike kuwa na rehema na mnyenyekevu, wakiwa tayari kutoa msamaha bila kuhitaji toba." (Worthington 2003: 51-52)

**b.** *Toba ni muhimu ili kufanya upatanisho na mtu mwingine.*

(1) Kwa sababu msamaha ni kitu cha muhimu ambacho wewe mwathirika unahitaji, ndani yako mwenyewe, ufahamu, na nafsi, mtu mwingine hahitajiki kuomba radhi kama sharti la wewe kutoa msamaha. Ikiwa toba inahitaji mtu mwingine atubu kwanza ili wewe usamehe, itakuwa ni *vigumu* au ili wewe usamehe, *hata kama ungehitaji* kama mkosaji angefariki, ameenda mbali, amepata ulemavu, au amekataa tu kutubu. Kwa kweli: "watu wanahitak a kusamehewa, na tutawajibika kama hatutasamehe" (**Math 6:12, 14-15; Luka 6:37-38**). Kama toba ya aliyekosa ingehitajika kabla ya sisi kuweza kusamehe, basi *sisi* tungeharibikiwa ikiwa mkosaji atakataa kutubu. "Na bado Mungu asingetuwajibisha kwa jambo ambalo hakuweka katika uwezo wetu." (Worthington 2003: 51)

(2) Kwa upande mwingine, kumsamehe mtu haimaanishi ni lazima uwe na mahusiano na yeye: kusamehe bila masharti mshirika wa biashara aliyekudanganya haimaanishi kubaki naye katika biashara; kumsamehe mtu unayeishi naye (pamoja na mume wako) anayekupiga, haimaanishi uendelee kuishi naye. *Kurudisha mahusiano* ndiyo maana ya upatanisho. Hiyo inahitaji kuanzisha upya *kuaminiana* na kujenga upya *kuaminika* kwa mkosaji. Mkosaji lazima *ajirejeshee* haki ya mahusiano. Ndiyo maana toba si sehemu ya muhimu kwa wewe kusamehe mtu lakini ni sehemu ya muhimu katika mchakato wa

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

upatanisho na mtu huyo. Kama ilivyoelezwa hapo mapema: *Inahitaji tu mtu mmoja kusamehe; inahitaji watu wawili kupatana.*[16]

**c.** *Toba ni muhimu ili kurejesha nafasi:* Hii ndiyo tafauti ya upatanisho. Ingawa kosa la mtu binafsi dhidi yako, mtu binafsi, anatakiwa kusamehewa bila masharti, dhambi hizo zinaweza kuwa na matokeo. Matokeo yake, ingawa unatakiwa kutendea kazi kwa kutumia mchakato wa msamaha wa REACH kumsamehe mtu aliyeiba fedha zako, au aliyebaka binti yako, au aliyekusababishia wewe maumivu mengine yoyote au jeraha, kumsamehe kwako yule mtu hakumwondoi kwenye mkondo wa sheria kwa kitendo chake; kwa hakika, anaweza akapata matokeo magumu (kuhukumiwa kifo, kufungwa, faini, fidia, aibu, kuondolewa kazini, n.k.) kwa ajili ya kile alichofanya. Kwa hiyo, katika **Math 18:15-20**, **1 Wakor 5:1-5,** na **2 Wakor 2:5-8** Yesu na Paulo wanaagiza kwamba washirika wa kanisa waliotenda dhambi wanatakiwa kunidhamishwa (lakini hitimisho ni mchakato wa urejesho) na kanisa ikiwa dhambi zao zimethiri kanisa.

**d.** *Toba ni muhimu ili kumwondolea mtu hatia na aibu.* Yote mawili aibu (uzoefu wa kibinafsi na hisia za kutenda mabaya, kudhalilika, kutengwa) na hatia (kujua ukweli kwamba upo kwenye kosa, na ni mkosaji) haitaanza kumwacha mkosaji mpaka atakapotambua, atakapokiri, na kutubu hatia. Kisha anaweza akaanza mchakato wa kurejeshwa kwa watu na jamii iliyotengana naye, aibu yake, pamoja na hatia yake, inaweza kupunguzwa au kuondolewa.

---

[16]Hiyo inaweza kuwa ni sababu nyingine kwa nini Mungu anatutaka tutubu na kuunganisha na hali ya Yeye kutusamehe sisi: msamaha wake kwa hakika hautuachi peke yetu, katika hali ya kusamehewa na pamoja na hayo kuwa nje ya mahusiano na yeye; bali, msamaha wake huturudisha katika mahusiano sahihi na yeye. Hiyo inahusisha yeye kutuchagua, kutufanya wana, kutukomboa, kutupa urithi na kutuweka muhuri kwa Roho Mtakatifu (**Waef 1:3-14**). Kama Smedes anavyoeleza, "ikiwa watu wanataka kusamehewa na Mungu, wanataka kuunganishwa na yeye wakati huo huo. Lakini Mungu anataka mwunganiko wenye uadilifu. Na toba siyo kitu kingine bali ni kuwa wakweli kuhusu kile tulichofanya kuvunja mwunganiko wetu na Mungu. Hii ndiyo maana mtu hawezi *kutarajia* kusamehewa na Mungu mpaka pale atakapotubu kwanza." (Smedes 1984: 92-93)

Kina cha Mungu kutusamehe sisi-ambako kunahusisha kurejeshwa kwetu katika mahusiano sahihi na yeye-imeelezwa kwa usahihi na Sande katika mazungumzo yake na mtu aliyekuja kutaka ushauri kwake, Rick, ambaye alikuwa akipata ugumu wa kutoa msamaha kikamilifu (na kupatana) na mke wake, Pam (ambaye alifanya uzinzi): "Ninaweza kuona kuchoka katika uso wake. "Mimi'nina hakika wote wawili mpo kwenye maumivu makali, Rick. Lakini sidhani talaka itamaliza hilo. Ninyi mtakanyaga tu aina moja ya maumivu kwa lingine. Kuna njia ya kuweka ndoa yenu pamoja na kuweka yaliyopita nyuma yenu kwa hakika. Lakini hautaipata kwa msamaha mtupu uliompatia Pam."

"Unamaanisha nini, 'msamaha mtupu?"

"Rick, fikiri kwamba ndiyo tu umeungamana dhambi yako mbaya sana kwa Mungu, na kwa mara ya kwanza akasema na wewe kwa sauti: 'Nimekusamehe, Rick, lakini siwezi kamwe kuwa karibu na wewe.' Ungehisije?"

Baada ya ukimwa wenye mshangao, akajibu, Ninafikiri nitahisi inawezekana Mungu hakunisamehe mimi kwa hakika."

"Lakini hivyo si sawasawa na wewe unavyomsamehe Pam?" Nikauliza.

Rick akatazama kwenye sakafu, anahangaika kutafuta jibu.

Kwa sauti ya chini, nikaendelea, "Fikiria badala ya Mungu kusema, Rick, Nimekusamehe. Ninakuahidi, kamwe sitafikiri kuhusu dhambi yako tena, au kuishi nayo au kutafakari juu yake. Ninaahidi sitaibua tena na kuitumia dhidi yako. Ninaahidi sitasema na watu wengine juu yake.Na ninaahidi sitaruhusu dhambi hii isimame kati yetu au kuzuia mahusiano yetu."

Baada ya kimya kirefu machozi yakaanza kulenga machoni mwa Rick. "Ningejua nimesamehewa kikamilifu . . . Lakini nisingestahili msamaha kama huo baada ya yale niliyomtendea Pam."

"Je ungestahili tena kuupata?" Nikauliza. "Msamaha wa Mungu ni zawadi ya bure iliyonunuliwa kwa ajili yako na Yesu kwa mauti ya msalaba. Hakupi msamaha kwa sababu umejistahilisha. Anakusamehe kwa sababu anakupenda. Unapotambua thamani ya msamaha na jinsi ambavyo hatustahili, utahitaji kumsamehe Pam kwa namna ile ile aliyokusamehe yeye." (Sande 2004: 202)

Kwa hiyo kama ilivyofafanuliwa hapo juu, kama vile ambavyo ipo tofauti kati ya Mungu na mtu, vivyo hivyo inaonekana tofauti kati ya msamaha wa kiungu na msamaha kati ya mtu na mtu. Pamoja na hayo kuna mpishano wa wazi kati ya msamaha na upatanisho: Rick anaelewa asili ya msamaha wa Mungu ambao ulimwongoza yeye kumwomba msamaha Pam kwa ajili ya uchungu na kukosa kumfurahia alioonyesha kwake pamoja na madai yake ya kuwa "amemsamehe" yeye. (Kwa kutumia misemo ya Worthington, Rick mwanzoni alikuwa ametoa "msamaha wa kihisia"; alipomwomba Pam amsamehe kwa ajili ya uchungu na kukosa kwake furaha, alikuwa amefikia hatua ya "msamaha wa kihisia" vile vile.) Kisha, hilo lilimsababishia Pam afunguke na kueleza hatia yake mwenyewe, aibu, na hofu, na hatimaye wakafikia kwenye urejesho wa ndoa (Ibid.: 203).

**B.** ***Maandiko hayahitaji toba kuwa masharti kwa ajili ya msamaha wa mtu kwa mtu***

1. Vifungu kadhaa (k.m., **Marko 1:14-15; 6:12; Luka 13:3; 24:47; Matendo 2:37-38; 1 Yoh 1:9**) vinaunganisha msamaha na toba. Ingawaje, mazingira hayo yote yanajadili msamaha wa *Mungu*, wokovu, na kurejeshwa kwa mwenye dhambi katika mahusiano yake sahihi na Mungu. Hakuna hata moja kati ya mistari hiyo inayodai mkosaji atubu kwanza kabla hajasamehewa katika mazingira ya msamaha wa mtu na mtu. Zaidi, hiyo yote inajihusiana na watu *wanao*taka kusamehewa, siyo na watu wanaohitaji *kufanya* jukumu la kusamehe.

**2.** Vifungu viwili pekee, wakati mwingine vimedai kufanya toba kuwa masharti kwa ajili ya msamaha wa mtu na mtu: **Math 18:15-20** *("Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye . . . na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru");* na **Luka 17:3-4** (*"Jilindeni; kama ndugu yako akikosa, mwonye;akitubu msamehe. Na kama akikukosa mara saba katika siku moja, na kurudi kwako mara saba, akisema, Nimetubu, msamehe").* Wakati mwingine mfano wa mwana mpotevu, **Luka 15:17-21** (*"Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena."),* inanukuliwa vile vile. Katika hayo matukio hakuna hata mmoja, pamoja na hayo, linalomhitaji mkosaji kutubu kabla hajasamehewa:

**a.** *Mtu analazimika kutofautisha kwa uangalifu kati ya nini kinaelezwa na nini kimeagizwa.* **Luka 15** na **17** *inaeleza* mazingira ambayo mkosaji alitubu. Maandiko hayo *hayasemi* kwamba mtu aliyekosewa anatakiwa kusamehe "kama, lakini kama tu" mkosaji atatubu. Vile vile, hayasemi kwamba mtu aliyekosewa *hata*kiwi kusamehe kama mkosaji *haja*tubu.

**b.** *Katika* ***Luka 15****, ona kwamba, ingawa mwana mpotevu "alizingatia moyoni mwake" na akaelezea toba yake, baba alidhihirisha msamaha wake hata kabla ya mwana kutamka maneno yake ya toba kwa baba* (**Luka 15:20**).[17] Angalia pia baba katika mfano huo alidhihirisha misamaha yote miwili "msamaha wa maamuzi" na "msamaha wa kihisia" (Worthington 2003: 53-54).

**c.** *Muktadha wa* ***Mathayo 18*** *kimsingi unaonekana kuhusisha kisa cha marudi katika kanisa, dhambi inayoathiri kanisa, na/au kurejeshwa kwenye ushirika au nafasi ya uongozi.* Ellingworth anaeleza kwamba nukuu ya Yesu katika **Yoh 20:23** "kwa hakika ni kwa ajili kuleta nidhamu katika jamii ya waaminio, na siyo kukataa kusamehe makosa ya mtu binafsi," na **Math 16:19** na **Math 18:18** "zinafana, lakini bila shaka inarejea kiujumla kuhusu maamuzi ya nini kinaruhusiwa na kukatazwa kati ya jamii kuliko msamaha peke yake" (Ellingworth 1992: 242). Kama ni hivyo, msamaha ni wa thamani, ni lazima, na ni sehemu ya muhimu katika mchakato wa urejesho. Tofauti kati ya hilo na binafsi, msamaha wa mtu kwa mtu imeonyeshwa na kifungu cha karibu kinachofuata, ikianzia katika **Math 18:21**, mahali Petro ameuliza "Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba?" Kristo *hakuwa* na haja kwamba mkosaji atubu kwanza kabla ili asamehewe "hata saba mara sabini" (**Math 18:22**).

**d.** *Hatimaye, sisi ni lazima tutambue katika fahamu zetu tofauti iliyopo kati ya kutoa msamaha na kupokea msamaha..* "Jambo la kutubu ni muhimu sana ili kupokea msamaha, lakini haina umuhimu wowote katika kutoa msamaha" (Jeffress 2000: 73). **Luka 15** na **17** inaelezea habari za watu waliohitaji kusamehewa; walielezea toba yao kama sehemu ya *kupokea* msamaha.

**C.** ***Msamaha hauwezi "kununuliwa" kwa toba, lakini msamaha usio na masharti unadhihirisha uhalisi, nguvu, uhuru, heshima na upendo***

**1.** Wengi hudhani kwamba "kama mtu aliyetukosea hatatubu, hastahili kusamehewa." Smedes anajibu hili kwa msisitizo mkubwa: "Kwa hakika, *hastahili* kusamehewa. Hakuna anayestahili. Na wala machozi yote katika bahari ya Neptune hayawezi kumpa haki au kumfanya astahili. Msamaha katika mazingira yoyote ni kwa ajili ya wale tu wasiostahili. Kuhuzunika kwa ajili ya makosa tuliyofanya hakutupi haki ya kusamehewa. Inawezaje? Hakuna kitu cha aina hiyo yaani haki ya kusamehewa. Msamaha hushuka tu kutoka kile ambacho wanatheolojia wanakiita neema-isiyogharimiwa, kibali usichostahili. Neema iliyogharimiwa siyo neema hata kidogo. Kwa njia isiyo sawa, ikiwa tunastahili kusamehewa, tusingeuhitaji." (Smedes 1984: 90-91)

**2.** Siku zote kuna upungufu kati ya kile anachodai aliyeumia na kile ambacho mkosaji anaweza kulipa. Katika kisa cha mwana mpotevu (**Luka 15**) hata baada ya mwana kusema, "Baba, Nimekosa," hakulipa

[17] Kwa kiwango hicho kwamba baba katika mfano wa Baba yetu wa Mbinguni, toba ni lazima kama ilivyojadiliwa huko nyuma. Hata hivyo, ona kwamba ni *baba* ndiye aliyeanzisha kwa *kukimbia* kukutana na mwanaye, hata wakati mwanaye "alipokuwa angali mbali." Vile vile, Baba yetu wa mbinguni ndiye aliyeanzisha katika kutuokoa sisi. Tazama, kwa mfano, **Yoh 1:12-13; 6:37, 44; Waef 2:8-9**.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

fedha alizochukua au miaka ya kuumwa moyo aliyosababisha; kwa hakika, mwana alishatumia vibaya urithi wake unaomwangukia. Hata toba ya kweli kabisa ya mbakaji haitarejesha ubikira uliopotea; toba ya kweli ya mwuaji haitarejesha uhai; toba ya kweli ya mtu aliyeng'oa jicho lako haiwezi rejesha kuona kwako. Toba haiwezi "kuvuka viwango"; ni upungwani kufikiri kwamba inaweza. Kwa hiyo siyo sahihi kudai mkosaji atubu kabla hujamsamehe.

**3.** Huwezi kumfanya mtu yeyote atubu mahali popote. Mkosaji anaweza akawa amekufa, au ameondoka, hawezi kutubu, ikiwa hafahamu kama amekukosea wewe, au tu hajali. Msamaha bila masharti huzingatia hayo. Haifanyi msamaha wako umtegemee mtu fulani atubu jambo ambalo lipo juu ya uwezo wako.

**4.** Msamaha usio na masharti ni kufanyia kazi mamlaka. Inakuweka wewe kwenye nafasi ya kuamua kutoa au kutotoa msamaha wewe mwenyewe. Kuhitaji mkosaji atubu kabla ya wewe kumsamehe kunakushusha wewe kwake. Kibaya zaidi, hilo linakufanya wewe umtegemee yule aliyekuumiza. Kuhitaji mkosaji atubu kwanza kabla ya wewe kumsamehe kunampa mkosaji nguvu ya kutawala moyo wako, ufahamu, na nia yako.

**5.** Msamaha usio na masharti unakuweka huru wewe dhidi ya mkosaji. Unakuweka wewe huru dhidi ya kufungwa kwenye yaliyopita, uovu, maumivu, na ubaya. Unakuweka huru kutoka kwenye hali tegemezi. Unakusaidia wewe kupona na kuendelea na maisha yako.

**6.** Msamaha usio na masharti huonyesha heshima kwa mtu mwingine. Kumsamehe mtu bila kumtaka atubu kwanza kunadhihirisha kwamba unamwona yeye kama mtu mwenye uwezo wa kubadilika. Inaweza kwa hakika kumpa motisha ya yeye kubadilika.

**7.** Msamaha usio na masharti ni kiwango cha juu cha kuonyesha upendo. Kama ilivyojadiliwa mapema, moja ya funguo "hisia kali" ambayo inasababisha kutosamehe ni hofu. Na bado Biblia inasema kwamba, "hamna hofu katika pendo; bali upendo wa kweli hutupa hofu njema" (**1 Yoh 4:18**). Kama asemavyo Jeffress: "ikiwa toba ni hitaji ili kutoa msamaha basi hiyo ina maana kwamba ni lazima tukutane na kila mtu aliyetukosea kabla ya kumsamehe kikamilifu. . . . Lakini tunataka kweli kutumia maisha yetu kutafuta kuombwa msamaha kutoka kwa kila aliyetuzunguka? Tunataka kuwahakikishia watu wawe wanakimbilia milimani wanapotuona tukiwaendea kama kila wakati tunataka 'kuongea kuhusu jambo binafsi? Na kwa umuhimu zaidi, je maisha hayo ya kukabili watu kwa namna hiyo hayapingani na mantiki ya upendo wa kikristo, upendo 'ambao hauweki kumbukumbu ya makosa' (1 Wakor 13:5 NIV)." (Jeffress 2000: 80)

**8.** Msamaha usio na masharti hufuata mfano wa Kristo. Yesu alitusamehe sisi hata kabla hatujatubu dhambi (tazama **Marko 2:3-12; Luka 7:36-48; 23:33-34; Yoh 8:1-11**). Kwa hiyo, tunapaswa kuwa tayari kusamehe hata kabla hatujaombwa msamaha.

## VII. Kupokea msamaha kwa ajili ya dhambi zetu tulizomkosea Mungu na watu wengine

### A. *Pokea na kupata msamaha wa Mungu kwa ajili yako*[18]

**1.** Kwa kuwa tunasamehe watu kwa sababu sisi tumesamehewa, ni muhimu kwanza *kupokea* msamaha wa Mungu kwetu katika mioyo yetu, ufahamu, nafsi na utu. Jeffress husema, "huwezi kutoa ambacho hujamiliki" (Jeffress 2000: 143). Kwa mantiki hii, ni muhimu "kuhisi" au "kuutendea kazi" msamaha wetu kutoka kwa Mungu. Smedes anaongeza, "Muunganiko kati ya kuhisi kusamehewa na nguvu ya kusamehe ni ufunguo wa mengine yote" (Smedes 1984: 120). Tunakiwa kuona hitaji letu wenyewe kubwa la msamaha. Tunatakiwa kuwa na uelewa sahihi wa Mungu na sisi wenyewe-utakatifu na wema mkamilifu wa Mungu, na wa dhambi ikaayo moyoni mwa kila mmoja wetu ambayo inaharibu kila sehemu ya utu wetu (k.m, **Mwanzo 5:1-3**; **Ps 51:5**; **Yeremia 17:9**; **Yoh 8:31-34**; **Warumi 3:9-18**; **6:6, 20-21**; **7:14-25**; **Waef 2:1-3**; **Tito 3:3**; **2 Pet 2:18-19**).

**2.** Tunahitaji kutafakari ni kwa *kiwango gani* tumesamehewa—wazo hilo linatakiwa liwe daima sehemu ya utambulisho wetu na jinsi tunavyojiona wenyewe. Huu uelewa kuhusu sisi wenyewe, na wa hitaji letu la, na kina cha, msamaha wetu wenyewe, inafanya iwe rahisi zaidi kuwasamehe wengine (na kungetufanya kuwa wanafiki kupindukia kama hatutasamehe wengine). Kama Kristo alivyoonyesha aliyesamehewa sana atapenda zaidi, na aliyesamehewa kidogo atapenda kidogo (**Luka 7:47**).

**3.** Tunahitaji kufahamu asili na kadiri ya msamaha wa Mungu kwetu. Mungu ametusamehe *kikamilifu na milele*—bila masharti, mashaka au kubagua.

**a.** *Biblia inatumia ishara kadhaa kutuonyesha ni kwa ukamilifu kiasi gani, na bila mashaka, au*

[18]Sehemu hii ni kwa misingi ya Jeffress 2000: 143-55 Smedes 1996: sura ya. 8, 14; na Worthington 2003: sura ya 3.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

*masharti yaliyofichwa au ubaguzi msamaha wa kweli wa Mungu ulivyo kwetu:*

(1) **Zab 103:12:** *"Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi."*

(2) **Isaya 38:17:** *"Kwa maana umezitupa dhambi zangu zote Nyuma yako.."*

(3) **Isaya 43:25:** *"Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako."*

(4) **Mika 7:19:** *"Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari."*

**b.** *Dhabihu ya Yesu mwenyewe kwa ajili yetu imesababisha msamaha wa daima wa dhambi zetu: [12] Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu. . . [14] Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa . . . [17] dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa.* (**Waeb 10:12, 14, 17**)

**c.** *Kama kweli tukifahamu kina cha hali yetu ya dhambi, ukubwa wa neema ya Mungu, na kiwango cha msamaha wetu, mwitikio wetu ungekuwa ni shukrani, upendo, unyenyekevu, na msamaha.* "Kwa sababu Mungu kwanza alitenda kwa upendo, huruma, na haki, mwitikio wa mkristo kwa alichofanya Mungu ilikuwa shukrani. Katika Ukristo, Mungu siku zote ndiye anayeanza kutenda. Baadhi ya watu wamejadili kuwa shukrani *ndiyo* hisia ya msingi kwa mkristo (Zab 50:14, 23; 1 Wathes 5:18)." (Worthington 2003: 63)

**d.** *Msamaha wa Mungu kwa dhambi zetu na makosa yetu ndiyo kielelezo ambacho kwa hicho sisi tunatoa msamaha kwa wengine:wa kudumu na na kikamilifu, bila ya masharti, kusitasita, au ubaguzi.*[19]

**B. *Kutafuta msamaha kutoka kwa wengine***[20]

**1.** Kama kweli tunaona na kuelewa uhitaji wetu na hali yetu ya dhambi, kiasi na kina cha msamaha wa Mungu kwetu, na hitaji letu la daima la msamaha wake kwa ajili ya dhambi zetu tunazoendelea kuzifanya, tunapaswa kirahisi kuhamasika kutafuta msamaha kwa watu ambao tumewakosea na kuwaumiza. Kwa hakika, kutafuta kwetu msamaha *kutoka kwa* wengine bila shaka ni moja ya hamasa kubwa sana inatufanya sisi kutoa msamaha *kwa* wengine. Pamoja na hayo, tunawezaje sisi kukataa kusamehe wakati sisi siyo kwamba tunaenda kwa Mungu ila *kwa watu wengine* ili kutaka msamaha kwao?

**2.** Kutafuta msamaha ni hatua ya kwanza kuelekea kwenye (kutengeneza mahusiano yaliyovunjwa na makosa). Kutafuta msamaha kunahitajika kufanyike mara tu baada ya kumkosea mtu-kwa namna hiyo, kuna muda kidogo wa mtu "kuwa sugu" dhidi yako na kwa mwili wote kutengeneza hali ya hisia ya kutokusamehe ndani ya mtu mwingine.

**3.** Kutafuta kusamehewa kunahusisha mlolongo wa hatua:

**a.** *Azimia kwamba unahitaji kuomba msamaha.*

(1) Ni kama tu ambavyo sisi "tunasamehe" matendo mabaya (ikiwepo hotuba) ya wale waliotukosea, kwa hiyo sisi tunatafuta msamaha tu kutoka kwa wale tuliowakosea kwa maneno yetu na kwa tabia zetu. Kule tu *kuwaza* mabaya, tamaa mbaya, au mawazo mengine mabaya dhidi ya mtu fulani hakutoshi kutufanya sisi kutafuta msamaha kutoka kwa mtu huyo. Sande anaeleza, "Ikiwa dhambi yapasa kuungamwa kwa watu wengine na kwa Mungu vile vile inategemea ikiwa ilikuwa ni 'dhambi ya moyoni' au 'dhambi ya jamii.' Dhambi ya moyoni inatokea katika mawazo yako tu na haiathiri watu wengine moja kwa moja. Kwa hiyo inahitaji kuungamwa kwa Mungu tu." (Sande 2004: 127)

(2) Katika kupambanua ikiwa tunahitaji kuomba msamaha au la, hatutakiwi kukana hatia yetu au kujifanya kwamba tulichofanya siyo kibaya sana. Tunapaswa kuzingatia mambo kama: (A) *Je tunaona aibu kwa kile tulichofanya?* (B) *Je tunahisi kujuta kwa*

---

[19]Namna moja yenye msaada sana ya kufikiri kuhusu msamaha wa wengine ni namna ambavyo Katekisimo ya Waangalikana katika *Kitabu cha Maombi ya Pamoja* kinavyoelezea sakramenti: "Sakramenti ni *alama ya nje nay a wazi ya neema ya kiroho ya ndani,* inayotolewa na Yesu Kristo kama hakikisho la kweli ambalo kwa hilo tunapokea neema hiyo" (*Kitabu cha Maombi ya Pamoja* 1979: 857). Huo mtazamo wa kusamehe wengine kwa hakika umeanzishwa na maonyo ya Kristo kuhusu mwunganiko wa msamaha wa mwanadamu na wa kiungu katika **Math 6:9-15; 18:21-35; Marko 11:25-26;** na **Luka 7:36-50**.

[20]Sehemu hii ni kwa mujibu wa Jeffress 2000: 155-64; Enright 2001: sura ya 14; na Chapman and Thomas 2006: *passim.*

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

*ajili ya tulichofanya?* (C) *Je tukio hilo linajirudia rudia katika fahamu zetu* (labda tunapojaribu kulihalalisha)? (D) *Je tunajilinganisha wenyewe na mtu tuliyemwumiza* (pengine tunajiambia wenyewe, "yeye ni mmbaya kama mimi nilivyo—au mmbaya zaidi!")? (E) *Tumesema uongo ili kufunika tulichofanya kwa ajili ya aibu?* (F) *Maisha yameathirikaje kutokana na kile tulichofanya* (hata kwa yale "madogo" njia za kutufanya sisi kuwa zaidi "wakali" au "wenye mioyo migumu")? (G) *Je tunalilia kuwa huru kutoka kwenye aibu na hatia ya makosa yetu?* (H) *Tumeshakiri dhambi zetu kwa Mungu na kupokea msamaha wake* (na kwa namna hiyo, ndivyo tunavyopaswa vile vile kutafuta msamaha kwa wale tuliowakosea)?

(3) Katika kisa cha mtu ambaye *hajui matendo yako* (kama vile mahusiano ya uzinzi na mtu fulani, ingawa mwenzi wako hajui) inaweza kuwa mtego. Jeffress anapendekeza angalau maswali matatu ya kujiuliza katika kisa hicho: (A) *Je malipizi ni lazima?* Ikiwa upande mwingine umepata hasara, na haujui ni nani amesababisha hasara hiyo, ni wajibu wako siyo tu kuomba radhi na msamaha bali na kufidia hasara; na kwa hakika kufidia hasara kutadhihirisha nia yako ya kuomba radhi na ya kutaka msamaha.

(B) *Kuna uwezekana gani kwamba kosa lako litajulikana?* Uhusiano wa miaka thelathini iliyopita unaweza usijulikane katika ndoa yako sasa, wakati huo huo uhusiano wa miezi sita iliyopita unaweza ukajulikana kwa mwenzi wako, na kusikia habari kutoka kwa mtu mwingine inaweza kuwa inaumiza zaidi kuliko kusikia kutoka kwako.

(C) *Je kukiri kwako kutasaidia au kutaumiza upande mwingine?* Anaongeza, "Hili ndilo jambo la-msingi. Wakati mwingine shauku yetu ya 'kukiri' inaweza kuwa kwa ajili yetu wenyewe zaidi. Wakati sisi tunaweza kujisikia huru kwa kupakua uchafu wetu kwa mwenzi wetu, yeye anaweza akapata mshtuko. Wakati mwingine upendo wa kujitoa dhabihu unatugharimu utayari wetu wa kubeba mzigo yetu wenyewe bila ya kumwomba mtu mwingine kutusaidia mzigo." (Jeffress 2000: 158-59)

**b.** *Kuomba msamaha.*

(1) Kumbuka kwamba "kuomba msamaha ni kumwomba mtu uliyemkosea *afanye kitu fulani:* kukufungua wewe kutoka kwenye deni lako" (Jeffress 2000: 161). Kuomba kukutana na mtu ni njia inayokubalika ya mawasiliano—kuongea na mtu mwingine ana kwa ana inamsaidia mtu mwingine kusikia hali ya sauti, kupata maelezo ya lugha ya viungo, na mwonekano wa usoni na kuuliza maswali ya ufuatiliaji, yote (au mengi) ya hayo yanazuiwa na mazungumzo kwa njia ya simu au barua.[21] Zaidi, kukutana ana kwa ana inasaidia kuonyesha kujaliwa kwa tukio, na kwa hiyo kuonyesha ukweli wa shauku ya kutaka msamaha. Hiyo hasa ni kweli kama, kwa sababu ya umbali utakaotembea au mazingira mengine, itakugharimu kukutana ana kwa ana. Kama Jeffress anavyoeleza, "Muda na kujitoa kunakohitajika kwa ajili ya juhudi hiyo inaweza kuwa kubwa, lakini siyo kitu ukilinganisha na furaha ya dhamiri safi" (Ibid.).

(2) Kuomba msamaha kunahusisha zaidi ya kusema tu bila ya kufikiria, "Nisamehe." Inahusisha kukubaliana na maumivu ya kushushwa kunakotokea tunapokiri kwamba tulikuwa na makosa. Hilo linaweza likawa gumu zaidi wakati mtu fulani aliye na mahusiano ya kimamlaka (k.m., mume, mzazi, au mwajiri) analazimika kujinyenyekeza na kuomba msamaha kwa mtu fulani anayemtegemea kwa karibu au mshirika (k.m.,mke, mtoto, au mwajiriwa). Hata hivyo, "Tukitaka kuwa huru, ni lazima tukubaliane na maumivu pamoja na huko kushushwa" (Enright 2001: 254).[22]

(3) Jeffress anaeleza namna nne za kumwomba mtu msamaha: (A) *Kataa kulaumu.* Hata kama upande wa tatu, au hata mtu ambaye unamwomba msamaha, kwa kiasi kikubwa ndiye aliyesababisha mgogoro, unatakiwa kujikita kwenye kosa lako mwenyewe. (B) *Tambua kosa ulilofanya.* Usijaribu kupunguza ukubwa wa kosa

[21] Kunaweza kukawa na utaratibu wa kipekee katika kila tamaduni au jamii wa kupanga kikao cha msamaha, kama vile matumizi ya ndugu wa familia, wazee wa kijiji, viongozi wa ukoo au kabila, viongozi wa kanisa, au wengine kama "watu wa katikati" au wawezeshaji. Kanisa lina wajibu wa kufanya au kujenga katika kusababisha msamaha.

[22] Tunapaswa kukumbuka (na kupata kutiwa moyo na) hili: Sisi kuwa watiifu kwa kristo. Zaidi, Kristo alipata uzoefu wa *kuaibika hadharani na kushushwa* kwa kudhihakiwa,kupigwa, na kusulubiwa uchi kwa dhambi ambazo *watu wengine* walifanya; tunapomwomba mtu mwingine msamaha, tunapata tu kushushwa *kibinafsi* (labda tukiwa tumetenda dhambi kosa kwa jamii, ambapo ukiri wetu ni lazima uwe kwenye hadhara) kwa sababu dhambi tuliyofanya *sisi* kwa mtu *binafsi*. Kweli, *"mtumwa si mkuu kuliko bwana wake"* (**Yoh 13:16**; tazama pia **Math 10:24; Luka 6:40; Yoh 15:20**).

ulilofanya au kuongea kiujumla tu. Mwenzako anajua ulichofanya; sasa yeye anataka kujua kama *wewe* unajua kikamilifu kosa lako. (C) *Tambua maumivu uliyosababisha.* Mwenzako anataka kujua kwamba wewe unaelewa maumivu aliyoyapata kutokana na matendo yako. Kutambua kwako hilo (au hata kusema huwezi kuamini maumivu [au uchungu au usumbufu] ambao jambo hili limekusababishia") itamfanya mwenzako awe tayari zaidi kukusamehe wewe. (D) *Mwombe mwenzako akusamehe.* Usikiri tu kosa ulilofanya kirahisi, bali hitimisha mazungumzo yako kwa kumwomba mwenzako kwa hiari akuachilie katika madai aliyonayo dhidi yako yanayotokana na kosa lako. Huwezi kudai msamaha; wala usitake kwamba eti mtu akusamehe wewe kwa ajili ya faida yake mwenyewe. Badala yake, Jeffress anashauri kuomba msamaha kwa kusema kitu kama: "Nimetambua kwamba nimekukosea kwa______. Nitafanya kwa kadiri niwezavyo ili kwamba kamwe nisirudie kufanya hili, ingawa ninatambua siwezi kufuta maumivu makubwa niliyokusababishia. Nilichofanya ni kosa, na simlaumu mtu yeyote ila mimi peke yangu. Leo ninakujia wewe kuomba ikiwa nitapata nafasi moyoni mwako ya kusamehewa kwa kile nilichofanya." (Jeffress 2000: 163)

(4) Chapman na Thomas wanafuata muundo wa aina hiyo hiyo wenye hatua-tano kwa ajili kudhihirisha kusikitika kwako na kuomba msamaha: (A) *Eleza majuto yako* (kwa mfano., "Nisamehe."); (B) *Kubali kuwajibika* (kwa mfano., "Nilikosea."); (C) *Fanya malipizi/toa fidia* (kwa mfano., "Nifanye nini ili kuweka sawa.?"); (D) *Fanya toba ya kweli* (kwa mfano., "Mimi' nisitende hivyo tena."); na (E) *Omba msamaha* (kwa mfano., "Tafadhali, utanisamehe mimi,?") (Chapman na Thomas 2006: *passim*).

(5) Sande ana kanuni yenye hatua saba, amabayo anaiita "A saba za Kuungama": (A) *Ongea na kila mtu aliyehusika.* Kiri makosa yako kwa kila mtu aliyeathirika moja kwa moja kutokana na kosa lako; (B) *Epuka maneno, Kama, Lakini, na Labda.* Neno "kama" (n.y., "Mimi' nisamehe kama nimefanya kitu fulani cha kukuhuzunisha wewe.") linaharibu ungamo lako kwa sababu linaonyesha kwamba wewe hujui kama umefanya au hujafanya kosa. Vile vile, kitu kama *yawezekana* nilikosa," *labda* ningejaribu kutumia bidii zaidi," "Nisingeshindwa kuzuia hasira yangu, *lakini* nilichoka," na "Mimi' ninaomba nisamehe, nimeumiza hisia zako, *lakini* ulinihuzunisha sana," kiondoa uzito wa sehemu iliyosalia ya "ungamo" na inaharibu uwezo wa kuwasilisha toba ya kweli; (C) *Kiri jambo mahususi.* Kadiri unavyoeleza kwa kina na kimahususi wakati unaungama, ndivyo inavyokuwa rahisi kupata mwitikio chanya; (D) *Tambua Maumivu*—Unahitajika kuonyesha kwamba unatambua vile ulivyomwumiza au ulivyomwathiri mtu mwingine; (E) *Kubaliana na Matokeo.* Kukubali kwa uwazi kupokea matokeo ya matendo yako, ikiwa ni pamoja na kufanya malipizi, inadhihirisha toba ya kweli; (F) *Badili Tabia Yako.* Mwambie mtu yule uliyemkosea vile ulivyojipanga kubadilisha tabia yako kwa siku za mbeleni; (G) *Omba msamaha (na Toa Muda).* Ukiwa umefanya kwa makini hatua hizo hapo juu, unaruhusiwa kuomba kwa wazi kusamehewa. Kuomba msamaha kunahamisha wajibu kwa mtu mwingine kuanza mwendo unaofuata. Hata hivyo, mtu asimshinikize mtu mwingine kufanya uamuzi wa haraka. Mtu aliyekosewa anaweza kuhitaji muda wa kufikiri, kuomba, na "kuchakata" kosa na ungamo. (Sande 2004: 126-34)

(6) Inawezekana ikawa tunatafuta msamaha wa mtu ambaye ameshafariki, hayupo tena, au amekataa kuongea nasi. Au, mtu anaweza akaitikia ombi lako la msamaha kwa kutofautiana, kwa namna hasi, au hata kikatili. Ingawa hiyo ni bahati mbaya, kama tukiwa wakweli na makini, kufanya yote katika kujuta, na kukubali kuwajibika kwa tulichokifanya na kufanya malipizi, tumetubu (tumebadilisha njia zetu), na kutafuta msamaha na kumaliza, bado sisi tunaweza kuwa na dhamiri safi kwa "kujua kwamba hata Mungu au mwingine yeyote anaweza kukutuhumu tu kwa kosa ambalo hatujajaribu kulirekebisha" (Jeffress 2000: 164).

**c.** *Kukua katika Kristo, na kuwa mtu mzuri zaidi, kama matokeo ya uzoefu wako.*

(1) Enright anashauri kwamba, kama matokeo ya makosa yetu na kutafuta kwetu msamaha, tunatakiwa: (A) *Tafuata maana katika makosa na kushindwa* (mafanikio yetu mara chache hutufundishwa sisi ukilingalinganisha na makosa yetu); (B) *Tambua kwamba sisi tuna nguvu kwa sababu ya kile tulichopitia* (kwa sababu ya ujasiri unaohitajika kukiri kosa na kumkabili mtu tuliyemwumiza, tutakuwa imara na wenye uwezo zaidi kukabiliana na makosa ya siku zijazo bila hofu); (C) *Tambua kwamba*

*hatupo peke yetu* (n.y., tunaweza kuhitaji msaada katika mchakato huu,[23] na tunatambua kwamba sisi ni kama watu wengine—hatutakuwa tena wenye kiburi na wenye kudhihaki wengine); (D) *Fanya maamuzi, na chukua hatua za lazima, za kutorudia kosa;* na (E) *Pokea uhuru kutoka kwenye hatia, majuto, na aibu ambao huletwa na kukiri kosa na kupokea msamaha.* Mambo haya yote yanatakiwa yatulete sisi karibu na Kristo na kutufanya tufanane na Kristo zaidi.

(2) Kwa kupitia Mambo yale yale matano ambayo Enright anayoshauri tunagundua baada ya kupokea msamaha yanapatikana kwetu kama, bila kosa letu wenyewe, mtu mwingine hawezi au hataweza kutusamahe. Kama tukitimiza wajibu *wetu*, uhuru na ukomavu unaotokana na kuomba msamaha, malipizi na kutubu havikaniki kwa sababu *mtu mwingine baki* hawezi kujiletea msamaha yeye mwenyewe.

(3) Sande anashauri kwamba tunaweza kupata uhuru kutoka kwenye dhambi zetu kwa "ku[fanya] kazi pamoja na Mungu ili atubadilishe mitazamo [yetu] na tabia huko mbeleni" (Sande 2004: 134). Anadokeza kwamba Mungu anataka kutusaidia tukue na kubadilika na kwamba hakuna dhambi au tabia katika maisha yetu ambayo hatutaweza kuishinda kwa neema yake. Wajibu wetu ni: (A) omba; (B) kujifurahisha wenyewe katika Bwana; (C) kujifunza; na (D) kuweka kwenye vitendo yale tunayojifunza (Ibid.: 134-35).

## UPATANISHO

### Rejea Muhimu za Maandiko

**I. Mungu ametupatanisha sisi na nafsi yake mwenyewe na kutupa huduma ya upatanisho (2 Wakor 5:16-21):** *16 Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena. 17 Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. 18 Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho, 19 yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. 20 Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. 21 Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*[24]

**II. Mungu amemaliza vikwazo vyote vinavyozuia upatanisho hata kati ya watu waliotofautiana sana (Waef 2:11-22):** *11 Kwa ajili ya hayo kumbukeni ya kwamba zamani ninyi, mlio watu wa Mataifa kwa jinsi ya mwili, mnaoitwa "Wasiotahiriwa" na wale wanaoitwa "Waliotahiriwa," yaani, tohara ya mwilini iliyofanyika kwa mikono—12 kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani. 13 Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. 14 Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga, 15 Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani, 16 Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba. 17 "Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu"; 18 Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. 19 Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu, 20 Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. 21 Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana, 22 Katika yeye ninyi nanyi*

[23] Kwa kuwa msamaha ni jambo la katikati kwa Ukristo, kanisa linatakiwa kuona sehemu ya wajibu wake katika kusaidia na kuwezesha mchakato wa msamaha na upatanisho. Kwa hakika, utafiti unaonyesha kwamba "watu wanaopta msaada kutoka marafiki katika makundi ya kanisani husamehe zaidi kuliko watu wa kanisani ambao hawajihusishi na vikundi" (Worthington, 2003: 70).

[24] Jina lililotafsiriwa"upatanisho" ni *katallagē,* ambalo lina maana ya "mabadiliko au kupatanishwa kutoka kwenye hali ya uadui kati ya watu na kuwa katika hali ya urafiki" (Zodhiates, 1993: *katallagē*; tazama pia Danker, 2000: *katallagē*, "kuanzisha upya kwa uhusiano ulioingiliwa au *kuvunjika*"). Neno liliotafsiriwa "kupatanishwa" ni lile lile *katallassō,* ambalo lina maana ya "kubadilika kwa ukatili kuwa uhusiano wa kirafiki, *patanisha*" (Ibid.: *katallassō*).

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

*mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho*. (Tazama pia **Warumi 10:12**; **1 Wakor 12:13**; **Wagal 3:28**; **Wakol 3:11**)

**A.** ***Mgawanyiko mkubwa kati ya watu katika Agano la Kale, na moja pekee wenye umuhimu wa kitheolojia, ni mgawanyiko kati ya Waisraeli na Mataifa; katika Kristo mgawanyiko huo haupo tena; kwa hiyo, watu wote ni sawa mbele za Mungu***

Kwa sababu uadui mkubwa na ukuta mkubwa unaotenga kati ya watu umeshaondolewa na Kristo, uadui mdogo na kuta zinazotugawa vile vile zimeondolewa; matokeo yake, katika Kristo hakuna vikwazo vya upatanisho kati ya makundi yoyote au watu.

**B.*Kusudi la Kristo ni kwamba sisi sote tuwe "mtu mpya" na tuwe na amani; kwa hiyo, kuishi kwetu kama wamoja na wenye amani kila mmoja kwa mwenzake ni "ishara ya nje inayoonekana"kwamba sisi kwa hakika tupo ndani ya Kristo.***

**C.** ***Kile alichofanya Mungu kwa ajili yetu (iliyoelezwa kwenye kifungu hapo juu), inatakiwa ifanye upatanisho kati yetu sisi na watu wengine kuwa kiini katika maisha yetu (kama Paulo alivyoeleza katika Waefeso wengine wote)***

Sande anafafanua jinsi gani mwitikio wetu kama wapatanishi na wafanya amani unavyotakiwa kutiririka kutoka kwenye kupatanishwa kwetu na Mungu kwa njia ya Kristo: "Barua ya Paulo kwa Waefeso kimsisitizo ililenga juu kufanya amani. Sura tatu za kwanza zinatoa maelezo matukufu ya mpango wa wokovu wa Mungu. Katika sura ya nne, Paulo anaanza kuelezea jinsi tutakavyoitikia kwa kile Kristo alichofanya kwa ajili yetu. Tazama kwa makini kile alichoweka Paulo katika mwanzo wa orodha yake ya matumizi ya Injili kwa vitendo: 'Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani (**Waef 4:1-3**). Neno la Kigiriki linatafsiriwa 'fanya kila juhudi' katika fungu hiki ina maana ya kujitahidi kwa nguvu, kwa makini, na kwa uangalifu. Ni neno ambalo amelitumia mkufunzi wa wapiganaji wakati alipotuma watu kupigana hadi kifo kwenye Coliseum: 'Fanya kila juhudi kubaki hai leo! Kwa hiyo pia mkristo anatakiwa kulilia amani na umoja. Bila shaka, bidii ya mdomoni na kujitahidi kwa juu juu katika upatanisho inaangukia chini sana ya kile Paulo alichokuwa nacho katika ufahamu wake." (Sande, 2004: 52)

**III. <u>Kupatanishwa kwetu mmoja kwa mwingine ni muhimu kiroho na kunahusiana na kumwabudu kwetu Mungu</u> <u>(Mathayo 5:21-26):</u>** [21] *"Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, 'Usiue,' na mtu akiua, itampasa hukumu.'* [22] *Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu 'akimfyolea ndugu yake,' itampasa baraza; na mtu 'akimwapiza,' itampasa jehanum ya moto.* [23] *Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako,* [24] *iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.* [25] *Patana na mshitaki wako upesi, wakati uwapo pamoja naye njiani; yule mshitaki asije akakupeleka kwa kadhi, na kadhi akakupeleka kwa askari, ukatupwa gerezani.* [26] *Amin, nakuambia, Hutoki humo kamwe hata uishe kulipa senti ya mwisho."*[25]

**A.** ***Katika kifungu Yesu anaweka wazi mwunganiko uliopo kati ya sisi kupatanishwa na watu wengine na kupatanishwa kwetu na Mungu.***

**B.** ***Kifungu kinadhihirisha umuhimu ambao Mungu ameuweka kwenye upatanisho kati ya watu-ni kuakisi "moyo wa ufalme"***

Dallas Willard anafafanua jinsi ilivyo ya ajabu kanuni ya **Math 5:23-24** kwa namna hii: "Wewe upo na wasimamizi wa hekalu mbele ya madhabahu, na tayari unataka kutoa sadaka kwa Mungu. Ni moja ya tendo la kiibada lililo takatifu sana katika maisha ya mtu mwaminifu. Uzoefu ni kwamba hili halitakiwi liingiliwe na lingine lolote isipokuwa baadhi ya mambo mengine muhimu zaidi ya kiibada yanayohitaji mwitikio wa haraka.

Ghafla, katikati kabisa ya yote hayo, unamkumbuka ndugu ambaye anakukasirikia. Ukitambua umuhimu wa hiyo nafsi kupata pumziko, na kuumizwa kutokana na tofauti iliyopo kati yako na yeye, unaacha hilo tendo. Unatoka na kumtafuta ili kupatana naye. *Hiyo* inafafanua uzuri chanya wa moyo wa kifalme.

---

[25]Neno liliotafsiriwa"kupatanishwa" katika **5:24** ni *diallassomai*. Ni sawa na maana ya *katallassō*, hiyo ni., "kurejeshwa kwenye hali ya kawaida kimahusiano au kuwa na amani na mtu fuulani, *kupatanishwa*" (Danker 2000: *diallassomai*).

Kupata matokeo kamilifu tunatakiwa kujiona wenyewe kana kwamba tunaolewa/tunaoa au tunabatizwa au tunawekwa wakfu kwa kazi fulani maalumu, kama vile mchungaji. Katika mchakato huo, tunatoka nje kutafuta upatanisho na mtu ambaye hata hayupo hapo. Hiyo ni picha ya upendo wa kifalme ambao ndiyo haki ya kifalme." (Willard 1997: 156)

**IV. Wakristo wameagizwa na Kristo na mitume wafanye kila wawezalo kuishi kwa amani wao kwa wao na pamoja na watu wote.**

**A.** ***Kristo alituamuru sisi kuwa na amani kila mmoja na mwenzake (Marko 9:50):*** *Chumvi ni njema; lakini chumvi ikiwa si chumvi tena, mtaitia nini ikolee? Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi.*

**B.** ***"Kila waraka katika Agano Jipya una amri ya kuishi kwa amani kila mmoja na mwenzake"*** (Sande 2004: 51).

**1. Warumi 12:18:** *Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote.* (Tazama pia **2 Wakor 13:11**; **1 Wathes 5:13**)

**2. Warumi 15:5-7:** [5] *Na Mungu mwenye saburi na faraja awajalie kunia mamoja ninyi kwa ninyi, kwa mfano wa Kristo Yesu;* [6] *ili kwa moyo mmoja na kwa kinywa kimoja mpate kumtukuza Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.* [7] *Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe.*

**3. 1 Wakor 1:10:** *Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*

**4. Wakol 3:15:** *Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani.*

**V. Kristo na Mitume walidhihirisha upatanisho kwa vitendo kwa maisha yao wenyewe.**

**A.** ***Kristo alidhihirisha upatanisho katika maisha ya hapa duniani. (Warumi 5:8-11):*** [8] *Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.* [9] *Basi zaidisana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.* [10] *Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.* [11] *Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeyesasa tumeupokea huo upatanisho.*

**B.** ***Kristo anaendelea kudhihirisha upatanisho katika jukumu lake kama kuhani mkuu (Waeb 7:23-25):*** [23] *Tena wale walifanywa makuhani wengi, kwa sababu wazuiliwa na mauti wasikae;* [24] *bali yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka.* [25] *Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.* (tazama pia **Warumi 8:34; 1 Yoh 2:1**)

**C.** ***Mitume walidhihirisha upatanisho katika maisha yao:*** linganisha **Math 20:20-24** na **Matendo 1:13-14; Matendo 15:36-40** with **2 Tim 4:11;** tazama pia **Filemoni 10-18**.

**VI. "Tunaposhindwa kutatua mgogoro sisi wenyewe, Mungu analiagiza kanisa liingilie na kuleta hekima, rasilimali na mamlaka yake ili kushughulikia tatizo (Math 18:16-17; Filemoni 4:2-3; 1 Wakor 6:1-8)"** (Sande 2004: 14).[26]

**A.** ***Kwa sababu kanisa ni mwili mmoja, wenye "viungo" vingi tofauti vyenye vipawa mbalimbali, ni muhimu kutambua na kuwafunza watu wanaoheshimika, wenye hekima, wenye ukomavu, wanume na wanawake wa kimungu katika kanisa wanaoweza kutumika kama washauri, wapatanishi, au wasuluhishi kuwezesha kati ya ndugu wengine kanisani (na kati ya wasio washirika wa kanisa pia).***

---

[26]Nyongeza F kwa mujibu wa Sande mpatanishi ni mtu anaye "tengeneza utamaduni wa amani katika kanisa lako." Taasisi yake, Huduma ya Upatanisho, ina maelekezo kuhusu mafunzo kwa ajili ya mpatanishi, kielimu, na shughuli za kipatanishi. Mawasiliano kwa ajili ya Huduma ya Upatanisho ni kama ifuatayo: anwani—P.O. Box 81130, Billings, MT 59108, U.S.A.; simu—(406) 256-1583; barua pepe—mail@HisPeace.org; tovuti—www.HisPeace.org.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**B.** ***"Wapatanishi wanaweza kufanya majukumu mbalimabali katika mgogoro"*** (Sande 2004: 191).

Sande anaeleza kwamba majukumu hayo ni: 1. Kuwasaidia watu walio na mgogoro kufanya uamuzi unaohitajika ili kurejesha amani; 2. Kuwezesha mawasiliano kwa kuutia moyo kila upande kumsikiliza kila mmoja wao kwa makini; 3. Kusaidia kutambua ukweli kwa kusikilizana kwa makini wao kwa wao, kwa kuuliza maswali yanayofaa, na kwa kuwasaidia watu walio na mgogoro kupata ukweli zaidi; 4. Kutoa ushauri wa namna ya kushughulika na tatizo (kama ilivyoelezwa katika Matthayo 18:17 na 1 Wakorintho 6:1-8); 5. Kuhimiza toba na kukiri kwa upande mmoja au kwa wote kwa kuonyesha tabia yoyote ambayo haiendi sawa na mafundisho ya Biblia; 6. Kuwezesha usuluhishi wa kibiblia kwa mambo yahusuyo vitu kwa kuelekeza pande hizo zilizo na mgogoro kufuata kanuni bora na mifano ya Maandiko; 7. Kushauri suluhu za vitendo kwa matatizo maalumu kutokana na ufahamu wao wenyewe na uzoefu wao (Ibid.).

## Kuelewa na Kutumia Upatanisho katika Maisha Yetu[27]

### I. Tofauti kati ya msamaha na upatanisho

**A.** ***Msamaha ni mwitikio wa mtu mmoja wa kimaadili kwa kosa la mtu mwingine; upatanisho ni kuja kwa watu wawili pamoja ili kurejesha uhusiano ambao umevunjika kwa kukosa uaminifu (i.e., kuondoa kikwazo cha kimaadili kwenye ushirika)***

"Inahitaji mtu mmoja kusamehe. Wanahitajika watu wawili kupatana tena.
Msamaha hutokea ndani ya mtu aliyejeruhiwa. Kupatana tena kunatokea kati ya watu.
Tunaweza kumsamehe ambaye kamwe hajasema samahani. Hatuwezi kupatana tena kikamilifu kama asipokuwa ametubu kikamilifu.
Tunaweza kusamehe hata kama hatumwamini mtu aliyetukosea mara moja na bila kutukosea tena. Kupatana kunaweza tu kutokea kama tunaweza kumwamini mtu aliyetukosea mara moja na kwamba hawezi kutukosea tena. Msamaha hauna kamba zilizofungamanishwa. Upatanisho una kamba zilizofungamano nao." (Smedes 1996: 27)

**B.** ***Tofauti kati ya msamaha na upatanisho***[28]

| | Msamaha | Upatanisho |
|---|---|---|
| *Nani?* | Mtu mmoja | Wawili au watu wengi |
| *Nini?* | Ni zawadi inayotolewa | Unagharimiwa, hautolewi bure |
| *Namna gani?* | Kubadilika hisia | Tabia kubadilika |
| *Wapi?* | Mwilini mwako | Kwenye mahusiano yako |
| *Namna ya?* | Mtindo wa msamaha wa Piramidi | Daraja la Upatanisho |

### II. Kwa nini upatanisho una umuhimu wa kibusara

**A.** ***Upatanisho ni ushahidi wa nguvu za Mungu, na unadhihirisha utii wetu kwa amri ya muhimu sana ambayo Kristo ametupa usiku kabla ya kusulubiwa kwake***

**1.** Katika usiku wake wa mwisho kabla ya kusulubiwa, Yesu alisema hivi: *Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.* (**Yoh 13:34-35**)

**2.** Bila ya upatanisho tutashindwa kuuonyesha ulimwengu *uthibitisha mmoja muhimu sana* wa sisi kwamba ni wanafunzi wa Kristo.

**B.** ***Upatanisho unatupa nguvu ya kupingana na uvamizi wa adui***

**1.** Kwa namna hasi, kushindwa kwa waamini kupatana kunawagawanya na kuwatenganisha, na hivyo kuwafanya kuwa kitoweo rahisi kwa mshambulizi ya adui.

**2.** Kwa namna chanya, waumini wanapoishi kwa amani na kwa maelewano kila mmoja na mwenzake huwa na umoja wa jeshi kuu, liwezalo kufanikiwa katika vita vya kiroho tunayohusika nayo (**Waef 6:12**), ili kwamba malango ya kuzimu isiweze kulishinda kanisa (**Math 16:18**).

---

[27]Sehemu hii kimsingi ni kutokana na Worthington 2003: sura ya 9-12; Jeffress 2000: sura ya 5; na Smedes 1996: sura ya 3; na kiwango cha juu zaidi na Enright 2001: sura ya 15.

[28]Chati ya ulinganisho inatokana na Worthington 2003: 171, Jedwali namba 9.1.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**C.** ***Kuishi kwetu kwa maelewano na, kwa baraka, na wengine matokeo yake ni Mungu kutubariki sisi (1 Pet 3:8-9):*** *[8] Neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu; [9] watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka.*[29]

## III. Jinsi ya Kupatanisha

**A.** ***Upatanisho hautokei ghafla, bali huchukua muda na hatua kadhaa***

**1.** Jeffress anaeleza hatua nne katika mchakato wa upatanisho (Jeffress, 2000: 115-23):[30]

**a.** *Toba.* Ingawa mmoja anaweza kumsamehe mtu ambaye kamwe hajakiri kuwa amesababisha jeraha, mara zote upatanisho wa mahusiano utahitaji utayari wa kukiri makosa na kutambua maumivu yaliyosababishwa; ili kwamba mahusiano ya mtu kwa mtu yaweze kupona na kujengwa kwenye msingi mpya ulio imara zaidi.

**b.** *Malipizi.* Kujaribu kurejesha kile kilichoondolewe kutoka, au kilichovunjika, katika mahusiano kunadhihirisha ukweli wa toba na umakini wa shauku ya kupata uponyaji wa mahusiano. Malipizi husaidia "kusawazisha uwanja wa mchezo," ili kwamba pande zote mbili zianze kufanya upya mahusiano yao katika misingi chanya (tazama Sande 2004: Nyongeza C, "Kanuni za Malipizi").

**c.** *Uponyaji.* Ili kuanzisha mahusiano na mtu fulani aliyetukosea, ni muhimu kuwa na uhakika kwamba mkosaji wetu amebadilika kwa hakika ili kwamba tusiathirike tena. Hiyo ndiyo maana toba ya kweli ni uthibitisho wa tabia iliyobadilika.

**d.** *Kujenga upya kuaminiana.* Wakati mwingine watu wengi wanaweza kuhitajika kusaidia kurejesha mahusiano (tazama **Wagalatia 6:1**). Mtazamo uliobadilika utasababisha kubadilika kwa maneno na matendo kwa mtu mwingine; hatimaye, mtu mwingine ataona kumaanisha kwetu. Inaweza kuchukua muda mrefu kujenga upya mahusiano ya kuaminiana mwanzoni. Kwa neema ya Mungu, hata hivyo, kushirikiana katika kutenda kwa pande zote mbili, hilo linaweza kutokea.

**2.** Bila shaka mtindo wa vitendo zaidi wa namna mchakato wa upatanisho *unavyotumika* ni ule wa Worthington. Ingawa anatumia misemo ya Jeffress na Sande, "toba, malipizi, uponyaji, na kujenga upya uaminifu" ambayo Jeffress ameyasema, na Sande "toba, kujipima mwenyewe, kukiri, na badiliko binafsi," zinaonekana katika utaratibu wa Worthington.

**B.** ***Daraja la Worthington la mtindo wa upatanisho***

Worthington ana mtindo wenye hatua nne, ambao anaufananisha na daraja, lenye hatua nne au matukio: uamuzi, mjadala, kuuondoa sumu, na kujitoa (Worthington 2003: ukura wa 9-12):




**1.** Amua. Kwanza hutangulia uamuzi, kwamba tunahitaji kupatana au la. Upatanisho huhitaji kwenda pande zote *mbili*, kwa hiyo pande hizo zinaweza kukwamisha katika hatua yoyote. Upatanisho unahitaji

[29] "Baraka" tunazoweza kupokea kutoka kwa Mungu zinahusiana na "tabia ya haki ambayo inaamriwa na Petro kwa [waaminio] inaonekana katika mstari wa 8-9a" (Grudem 1988: 147). Ingawa baadhi ya waliotoa maoni yao wanakoleza "baraka" wakimaanisha wokovu wa mtu wa siku ya mwisho, wazo lenye nguvu pia linaweza kutolewa kwamba kile alichomaanisha Petro ni kwamba kuishi maisha ya maelewano na kuwabariki wengine kama malipo kwa mabaya kunaleta baraka kutoka kwa Mungu katika maisha ya sasa (cp., Michaels 1988: 178-79, pamoja na Grudem 1988: 148-49).

[30] Sande ana mtindo wa mchakato wa urejesho wa aina hiyo wenye hatua nne:: (1) toba; (2) kujipima mwenyewe; (3) kuungama; na (4) badiliko la kibinafsi (Sande 2004: 118-35).

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

muda, juhudi, unyenyekevu, na hatari ya kuumizwa tena au kutumiwa kwa maslahi binafsi na mtu mwingine.

**a.** *Mtu anaweza asitake kupatana ikiwa:* (1) anapenda kuwa mbali na haoni sababu ya kuanza upya mahusiano; (2) una hatarisha afya au si salama kufanya hivyo (kuna hatari ya kuumizwa kimwili au maumivu mengine); (3) mmoja amekuwa akikosa uaminifu mara kwa mara na huonyesha toba au majuto kidogo au haonyeshi kabisa; (4) maumivu na jeraha, sasa kwa kiwango cha chini, ni makubwa sana; (5) mmoja amekufa, hayupo, au kwa sababu nyingine haiwezekani kupatana.

**b.** *Watu huamua kupatana kwa sababu:* (1) hawahitaji kukubali kushindwa katika mahusiano; (2)wanathaminiana kila mmoja na mwenzake na katika mahusiano; (4) hawako tayari kurudi kwenye *hadhi yao ya kawaida* lakini wanataka mahusiano imara na yaliyo bora zaidi; (5) wanaamini kwamba kupata upatanisho ni dhahiri kutakuwa na matokeo chanya zaidi kuliko kutofanya chochote.

**c.** *Ni lazima tuamue jinsi ya kupatana. Upatanisho hutokea kwa njia mbili:*

**(1)** <u>Upatanisho mara nyingi huja *kikamilifu*, bila ya pande husika kujadiliana kwa wazi. Upatanisho usio wazi unahusisha:</u> kuacha ukali; kuja pamoja (nayo ni, kwa ajili ya jukumu la pamoja); kuungana pamoja na (au kuunganishwa pamoja na) mtu wa tatu kwa ajili ya shughuli mbalimbali; kuwa na mtazamo chanya na kukamilishana mmoja kwa mwingine; tukitambua umoja wetu na Kristo, ambayo inaweza kusaidia kuvunja "kuta za mgawanyiko" za ufahamu na za kihisia" (**Waef 2:14-16**).

**(2)** <u>Upatanisho *ulio wazi* unatokea wakati pande husika zinapokuja pamoja kushughulikia kipekee tatizo na kurejesha uhusiano uliovunjika.</u>

**(A)** *Ingawa baadhi ya watu hufikiri kwamba **Math 18:15-20** ni aina fulani ya "sheria" inayolazimisha kuwa na mazungumzo binafsi na ya siri na mtu aliyetukosea kabla ya kuwaomba wengine kujihusisha na hali hiyo, sivyo ilivyo.* Yakobo (**Mwanzo 32-33**), Abigaili (**1 Samweli 25:18-35**), Ayubu (**2 Samweli 14:1-23**), na Barnaba (**Matendo 9:26-27**) wote walihusika kwa niaba ya wengine, au waliwaomba wengine kujihusisha, ili kuleta upatanisho kabla ya pande husika zilizo na uhusiano uliovunjika kukutana peke yao.

**(B)** *Katika kujua jinsi ya kuanza mchakato wa upatanisho ulio wazi:* "Mazungumzo binafsi mara zote ni mazuri zaidi, lakini kwa visa baadhi kuhusisha watu wengine moja kwa moja itakuwa ni vizuri zaidi. Kuna hali kadhaa ambazo zinaweza kudhihirisha ukweli huo leo:

Wakati unahusika na mtu anayetoka kwenye utamaduni au desturi ambayo ni kawaida kutatua matatizo kupitia watu wa katikati kama vile wawakilishi wa familia au viongozi wanaoamiwa

Wakati unaenda kwa mtu fulani wewe mwenyewe na kibinafsi ni wazi kwamba hawataweza kuonekana machoni kwa wengine;

Wakati pande husika wanaweza kuhisi kuogopeshwa na mtu mwingine, labda kwa sababu ya ujuzi wa kuzungumza au nafasi katika mamlaka au ushawishi;

Wakati mtu mmoja amenyanyaswa na mwingine na kuna uwezekano kwamba mnyanyasaji atatumia mazungumzo ya siri kumrubuni au kumnyamazisha mtu aliyenyanyaswa;

Wakati upande wa tatu alio na uhusiano wa karibu kuliko wewe ulivyo na mtu anayeweza kukutwa na dhambi, na huo upande wa tatu upo tayari kuibua jambo pamoja na mkosaji." (Sande, 2004: 146-47)

**d.** *Ni lazima kuamua ni wakati gani tupatane.* Msamaha wa Maamuzi na Kihisia unaweza kufanyika kwa haraka wakati mwingine; upatanisho karibu mara zote huhitaji kipindi cha muda. Wakristo wanatakiwa kutafuta fursa za kuanzisha mchakato wa upatanisho. Kabla ya kuanzisha upatanisho *ulio wazi*, tunapaswa kutathmini nia zetu wenyewe na hali za ufahamu na hisia (je sisi tuna msongo sana? Tuna hasira?—bila shaka ni muhimu kuomba na kushughulika na hayo kwanza). Tunahitajika kumtathmini mtu mwingine na mazingira, na kuomba kwa ajili ya uongozi wa Mungu. Pamoja na hayo tunapaswa siku zote kutenda kwa namna inayoendana (na inayowezesha) upatanisho *usio wa wazi*.

**2.** <u>Jadiliana.</u> Mara uamuzi unapofikiwa, pande zinazohusika zinahitajika kuja pamoja na kujadili uhusiano wao, mgawanyiko ukiotokea kati yao, na jinsi ya kurejesha urafiki au uhusiano mzuri.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

**a.** *Utaratibu mzuri zaidi wa kukutana na kuongea na mtu mwingine ni kubadilisha mtazamo-kujenga "mtazamo laini."* Mtazamo mlaini husaidia *kuongea maneno malaini*, na hiyo ni muhimu kwa ajili ya upatanisho na mtu mwingine. Mtazamo laini una sifa ya rehema na unyenyekevu.

**b.** *Utafiti unaonyesha kwamba katika visa vingi, ukiacha kile ambacho kinaweza kuwa kweli katika "hali ya kawaida"pande zote mbili zinajiona kama waathirika na upande mwingine kama mwenye wajibu; pande zote mbili zinaweza kuja zimejiandaa kumsamehe mwingine, lakini hawako tayari kabisa kusamehewa* (Worthington 2003: 191). Katika visa hivyo, pande zote mbili mara zote wana makosa. Mara zote, mtu aliye na *kosa dogo* (lakini ndiye anayetaka kurejesha mahusiano) anaweza akaanzisha mchakato kwa kumwendea mtu mwingine na kuungama makosa yake mwenyewe ambayo yaliharibu mahusiano (mtu aliyekosa zaidi anaweza akawa na aibu sana kuanzisha mchakato). Bila kujali ni nani kaanzisha mchakato, kuzungumzia mchango wako mwenyewe kwenye tatizo hufanya mambo mawili: (1) ni 'kufuata mafundisho ya Yesu' katika **Math 7:3-5** ku "ondoa boriti katika jicho lako mwenyewe" kabla hujashughulika na "kibanzi katika jicho la ndugu yako"; na (2) "ungamo lako wakati mwingine litamtia moyo mtu mwingine akiri dhambi zake" (Sande 2004: 158). Sande anaita hii kwamba "Matokeo ya Dhahabu," ambayo yanafanana na Sheria ya Dhahabu (ambayo inatutaka sisi kuwatendea wengine kama tunavyotaka sisi tutendewe): "Matokeo ya dhahabu husema kwamba, *siku zote watu watatutendea sisi kama tunavyowatendea wao.* Kama tunawalaumu wengine kwa ajili ya tatizo, mara zote wao nao watatulaumu. Lakini kama tukisema, 'Nilikosa,' inashangaza ni mara ngapi mwitikio utakuwa, Lilikuwa kosa langu pia."' (Ibid.: 78)

**c.** *Ungamo lako kwa mtu mwingine humchokoza mtu mwingine kufanya angalau ukiri "usiotoka moyoni" unaweza ukaanzia hapo, na kurejea tena kwa mtu mwingine au uliza maswali ili kuibua jambo kwa kina zaidi.* Kuitikia kwa ukiri usiotoka moyoni kama, "Nathani hata mimi nilitumia hasira," au "Vema, hayakuwa makosa yako peke yako," Sande anashauri tuitikie kama vile: "Ninashukuru kwa kukubali kwako kwamba ulikuwa na hasira, Bob. Nikueleze hali hiyo ilisababisha hisia gani kwangu?"; "Ninashukuru kwa wewe kusema hivyo. Unafikiri ulikosea nini?"; au "Kwa nini unafikiri nilichanganyikiwa?" (Ibid.: 158).

**d.** *Katika kujadiliana na mtu mwingine, katika dhamiri yako inabidi uchukuliane na maelezo ya kina.* Jaribu kumpatia mtu mwingine mazingira yasiyo na mashaka. Rudia kwa muhutasari alichosema ili kwamba wote wawili mhakikishie yeye mnamwelewa vema. Uwe sahihi katika matarajio (kumbuka: upatanisho unaweza kuchukua muda mwingi na juhudi). Sisitiza sababu chanya za mtu mwingine zinazoonyesha kwamba sababu moja ya kuumizwa siyo kwamba yeye mara zote hutenda kwa jinsi hiyo. Jaribu kuepuka kuangukia kwenye mtego wa kukana kwamba hujafanya jambo lolote baya, au kutetea kila tendo ulilofanya kwamba ni sahihi, na wa kumlaumu mtu mwingine-hilo litapelekea mabishano zaidi. Sikiliza maelezo ya mtu mwingine na, na unaposema kwa nini ulifanya ulilofanya, jaribu kuepuka kumlaumu mtu mwingine (badala yake, elezea kwamba ulikuwa na hasira, au uliumia, n.k. bila kuongezea kwamba hasira yako ilikuwa sahihi kwa sababu ya mtu mwingine alifanya "hilo litokee").

**e.** *Hatimaye, utahitaji kufikia kusamehe na kukubali kusamsahe kila mmoja.* Utahitaji kujikita katika kubadili tabia yako mwenyewe, na siyo ya mtu mwingine. Utatakiwa kukubaliana na mpango wa kurejesha mahusiano.

**3.** <u>Ondoa sumu.</u> Mahusiano yanavunjika kwa sababu ya usaliti au majeraha mengine, ni kama sumu kuingia mwilini.

**a.** *Tunahitaji kujitenga wenyewe kutoka kwenye uhusiano na hiyo sumu.* Kwa hiyo, tunahitaji kushughulika na sisi wenyewe na kuondoa uchungu katika nafsi zetu tunapoungama; kama Mungu ametusamehe sisi, na kuchukua dhambi yetu na uchungu kwake yeye mwenyewe, hatuhitaji tena kubeba mzigo hatutabeba tena mzigo ule.

**b.** *Sisi vile vile tunatakiwa kuondoa sumu kutoka kwenye uhusiano.* Utafiti unaonyesha kwamba ndoa (na mahusiano mengine) inakisiwa unavunjika katika hatua nne: (1) <u>Ukosoaji:</u> kwanza katika ufahamu, kisha kwa maneno; (2) <u>Kujitetea:</u> kwanza katika ufahamu, kisha kwa maneno (hali ina sifa ya "kujibu kwa ukali" kwa mkosoaji, na huzalisha mabishano); (3) <u>Kutokubaliana:</u> ambapo kukosoana na kujitetea kunazalisha matendo halisi au tabia za mtu, kutokukubaliana kunaelekezwa kwa mtu mwingine yeye mwenyewe; (4) <u>Kuweka ukuta wa mawe au kupamabana:</u> ili kuepuka kuumizwa mtu anajitoa na kuugeuza moyo wake kuwa "ukuta wa mawe" au zaidi vita vya wazi, iliyobuniwa ili kumwumiza mtu mwingine (kiufahamu, kihisia,

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

au kimwili) inatokea. (Worthington 2003: 227)[31]

**c.** *Tafiti pia zinaonyesha kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya nguvu na furaha ya ndoa na uwiano wa mawasiliano chanya na hasi.* Kama wanandoa wana mawasiliano chanya 10, au 7, au hata 5 kwa kila mwasiliano hasi moja, mra zote wana furaha. katika 5:1, hata hivyo, mabadiliko ya ghafla hutokea: juu ya kiwango cha 5:1, kwa ujumla watu huyatazama mahusiano kwa mtazamo chanya. Zaidi, kama wanandoa wana uwiano ulio chini ya 5:1 mara zote siyo 4:1, bali hushuka kwa kasi sana hadi 1:1 au hata 1:2. (Worthington 2003: 227-28)

**d.** *Wazo la kuondoa sumu ni kurejea mchakato: nayo ni, kufanyia kazi tabia, maneno, na mawazo ndani ya dhamiri ambayo yanaelekea kwenye mwelekeo sahihi kutoka kwenye kuweka kuta za mawe, au vita kurudi kwenye kutokubaliana; kutoka kwenye kutokubaliana hadi kwenye kujitetea; kutoka kwenye kujitetea hadi kwenye kukosoana; kutoka kwenye kukosoana hadi kwenye hali ya kawaida.* Katika kufanya hivyo tunaweza kuangalia ishara zinazotuambia ikwa tunatia sumu, kuliko kuondoa sumu, kwenye mahusiano: (1) tunaleta maumivu yaliyopita, kuliko kushughulikia maumivu ya sasa; (2) tu wakali kupindukia tunapojibizana na mtu mwingine; (3) tunamshambulia mtu, kuliko kusimamia jambo; (4) tunasikia uchungu tunapoongea (5) hatuwezi kuachilia maumivu yaliyopita.

**4.** Jitoe. Hatimaye sisi tunaweza kufikia hatua ya urejesho, inayohitaji kujitoa kwa mtu mwingine na kwenye mahusiano.

**a.** *Tunafikia hili wakati tunapoacha kuendelea kuumia juu ya kosa; badala yake, tunatatua tatizo kwa kujifunza kutoka kwenye maumivu.* Tunaona jinsi ambavyo hili limetubadilisha sisi na, kwa hakika, limetufanya kuwa mtu mzuri zaidi. Tunafikia kiwango cha kujitoa tunapojenga upendo. Tunaelewa jinsi mtu mwingine anaweza akahisi kutothaminiwa na kuthaminiwa, yote mawili kupendwa na kutopendwa. Kisha tunafanya vitu hivyo ili kutokumdharau mtu mwingine, lakini kumthamini kwa namna chanya na kudhihirisha upendo wetu kwake. Hivyo, tunapunguza mwingiliano hasi na kuongeza mwingiliano chanya kati yetu, tukijaribu kuona mwingiliano huo kwa mtazamo wa huyo mtu mwingine.

**b.** *Kuongeza uwiano wa mwingiliano chanya na kuondoa mwingiliano hasi kunahitaji kumjua mtu mwingine vema na inahitaji huruma.* Inahitaji kufahamu namna ambayo mtu mwingine anavyohisi kwa uzuri zaidi uzoefu wake wa kupendwa. Njia za kudhihirisha upendo zinaweza kuhusisha: (1) maneno ya kupendwa na uthibitisho; (2) mguso wa kimwili na urafiki; (3) kutumia muda na mtu; (4) matendo ya huduma ya upendo; (5) zawadi ya upendo. (Chapman, 1995: *passim*) Tunatumia yale maelezo ya upendo ambayo mtu mwingine anayathamini kipekee. Kwa kifupi, kwa asili, kwa njia ya mchakato wa upatanisho tunafikia kumfahamu mtu mwingine kwa dhamiri na kuishi kama iwapasavyo wakristo, kwa nia na Roho wa Kristo, vile tunavyopaswa kuwaelewa watu na kuishi, nyakati zote, katika mahusiano yetu yote.

## NUKUU ZILIZOTUMIKA


Aland, Barbara, Kurt Aland, Johannes Karavidopoulos, Carlo Martini, and Bruce Metzger, eds. 2001. *The Greek New Testament,* 4th rev. ed. Stuttgart: Deutsche Bibelgesellschaft.

Alcorn, Randy. 2009. *If God Is Good.* Colorado Springs, CO: Multnomah.

*The Book of Common Prayer.* New York: Seabury, 1979.

Carson, D. A. 2002. *Love in Hard Places.* Wheaton, IL: Crossway.

Chapman, Gary. 1995. *The Five Love Languages.* Chicago: Northfield.

Chapman, Gary, and Jennifer Thomas. 2006. *The Five Languages of Apology.* Detroit: Thorndike.


[31] Mwendelezo huu unaendana na mtazamo wa Sande kwamba mzizi wa mgogoro ni "matakwa yasiyofikiwa katika mioyo yetu," ambazo pia zinafuata mchakato wa hatua nne: (1) Ninatamani—mgogoro huanza na aina fulani ya tamaa (ambayo, yenyewe, inaweza kuwa na maana au haina maana; (2) Ninahitaji—tama isiyofikiwa inakuzwa, na inageuka kuwa hitaji "ambalo ni lazima lifikiwe ili kuridhika na kutosheka," na inaweza kuelekea kwenye uchungu, kinyongo, na kujihurumia linazidi kutokufikiwa; (3) Ninahukumu—wakati wengine wanashindwa kutimiza tamaa yetu na kuishi kulingana na matarajio yetu, tunawakosoa na kuwahukumu wao katika mioyo yetu kama siyo kwa maneno yetu; (4) Ninaadhibu—mtazamo wa kuhukumu hutupeleka kwenye mtazamo wa kuhukumu unaotuongoza kwenye hisia za kutafuta jinsi ya wazi au isiyo wazi ya kuwadhibu watu na kuwalazimisha kufanya matakwa yetu . (Sande, 2004: 102-09)

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Danker, Frederick W., ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature,* 3d ed. Chicago: University of Chicago Press.

Ellingworth, Paul. 1992. "Forgiveness of Sins." In *Dictionary of Jesus and the Gospels,* ed. Joel Green, Scot McKnight, and I. Howard Marshall, 241-43. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Enright, Robert. 2001. *Forgiveness Is A Choice.* Washington, DC: American Psychological Association.

Grudem, Wayne. 1988. *The First Epistle of Peter (TNTC).* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Jeffress, Robert. 2000. *When Forgiveness Doesn't Make Sense.* Colorado Springs, CO: Waterbrook.

Klassen, Daniel. n.d. *The Forgiveness Workbook.* Thunder Bay, Ontario, Canada: Lakehead University.

McCullough, Michael. 2000. "Forgiveness as Human Strength: Theory, Measurement, and Links to Well-Being." *Journal of Social and Clinical Psychology* 19, no. 1: 43-55.

Michaels, J. Ramsey. 1988. *1 Peter (WBC).* Nashville, TN: Thomas Nelson.

Sande, Ken. 2004. *The Peacemaker,* 3rd ed. Grand Rapids, MI: BakerBooks.

Smedes, Lewis. 1984. *Forgive and Forget: Healing the Hurts We Don't Deserve.* San Francisco: Harper & Row.

_______________. 1996. *The Art of Forgiving.* Nashville, TN: Moorings.

Solzhenitsyn, Aleksandr. 1985. *The Gulag Archipelago 1918-1956.* Translated by Thomas Whitney and Harry Willetts. Abridged by Edward Ericson, Jr. New York: Harper & Row.

Willard, Dallas. 1997. *The Divine Conspiracy.* New York: HarperSanFrancisco.

Witvliet, Charlotte vanOyen, Thomas E. Ludwig, and Kelly L. Vander Laan. 2001. "Granting Forgiveness or Harboring Grudges: Implications for Emotion, Psychology, and Health." *Psychological Science* 12, no. 2: 117-23.

Worthington, Everett. 2001. *Five Steps to Forgiveness.* New York: Crown.

_______________. 2003. *Forgiving and Reconciling.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Zodhiates, Spiros, ed. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* rev. ed. Chattanooga, TN: AMG.

## NYONGEZA

### Mfano wa Msamaha wenye msingi wa maamuzi kwa ajili ya urejesho wa Ndoa na Mahusiano ya Kifamilia[32]

Mfano huu umeandaliwa kwa ajili ya wanandoa wakristo. Hata hivyo, unaweza kutumiwa na wakristo wanaokutana na matatizo katika mahusiano ya aina nyingine. Unaweza ukawa na msaada pia kwa wasio wakristo, lakini siyo sana kwa sababu kanuni zake ni za kibiblia ambazo zinaweza zisikubalike kwa wale wasio wakristo.

Kikao cha msamaha kinachohusisha mshauri nasaha na wanandoa kwa kawaida ni kirefu (angalau saa tatu kwa kiwango cha chini) na kina hatua 13. Hizi hatua zimepangwa katika sehemu tatu: **(1)** kutoa maana na maandalizi (**Hatua ya 1-3**), ambayo inahusisha mjadala kati ya mshauri nasaha na mwanandoa; **(2)** kutafuta na

---

[32]Mtindo huu unatokana na rasimu za makala zifuatazo: Frederick A. DiBlasio, "Maandiko na Msamaha: Kujihusisha na Wanandoa wa Kikristo na Familia," *Ndoa na Familia: Gazeti la Kikristo 2* (1999): 247-58, na Frederick DiBlasio na Robert Cheong, "Upendo wa Kikristo na Msamaha katika Ushauri wa Ndoa: Nadharia na Vitendo" (Iliyotolewa ma na waandishi kwa *Ndoa na Familia:Gazeti la Kikristo,* katika machapisho).

Kwa kuongezea, ECLEA katika tovuti yake inayo (www.eclea.net) yote mawili *Maelekezo na Mwongozo wa Kiongozi,* na *Maelekezo ya Mshiriki* kwa ajili ya kozi ya kukuza msamaha ya Everett L. Worthington, *Kupata Msamaha: Masomo sita ya Kivitendo ya Kufanyika Mkristo mwenye kusamehe zaidi.* Dr. Worthington ametoa ruhusa ya kupakua mafunzo haya, kuchapishwa, na kutumiwa bila malipo.

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kutoa msamaha (**Hatua ya 4-12**)—baada ya mwanandoa mmoja kumaliza hatua zote kati ya hatua ya 4-12 mwanandoa mwingine huanza; na **(3)** kikao huisha kwa tendo la maadhimisho ya kiibada (**Hatua ya 13**). Mwanandoa bila shaka atahitaji kupata ushauri nasahau siku zijazo baada ya kikao cha msamaha, lakini umalizaji wa mafanikio wa kikao kirefu cha msamaha kinatakiwa kupunguza idadi ya vikao vingine vya ushauri nasaha.

**Hatua ya 1:** *Maana ya msamaha hujadiliwa.* Mshauri nasaha anapata ruhusa ya kuongea kuhusu maana ya msamaha, kutoka kwa washauriwa kwa kuwa ni kiini cha imani. Wote waongee kuhusu maana ya msamaha. Mshauri nasaha hujadili nini Biblia inasema kuhusu msamaha na upendo. Mshauri nasaha atajikita kwenye utaratibu unaotegemea maamuzi. Mshauriwa ni lazima akubali kuwa uamuzi wa kusamehe hauhusishi ufahamu wa kuachilia na hitaji la kutolipa kisasi, bali pia unahusisha matendo ya msamaha ya kujikana mwenyewe na kupenda kama Kristo alivyofanya. Kuwaelekeza mwanandoa kwenye maandiko ni muhimu, kwa kuwa wakristo wengi wanataka mawazo yao, maneno na matendo yaende sawasawa na Maandiko.

**Hatua ya 2:** *Nia ya kila mtu kuwa na fursa ya kutafuta msamaha kwa ajili ya matendo yake yasiyo sahihi hujengwa.* Wenzi huwa na fursa ya kuungama makosa yao kila mmoja kwa mwenzake mbele ya mshauri. Nia siyo kutetea matendo yao, au kuwashambulia wenzi wao kwa makosa yao, lakini kujielekeza kwenye madhaifu yao wenyewe na kutubu kwa ajili ya makosa yao. Mshauri anaweza akasema kitu kama: "Tunahitaji kuweka mwongozo kwa ajili ya kikao chetu. Wenzi mara nyingi huja na mambo mengi kwenye ushauri kuhusu tabia inayoumiza ya mwingine, lakini mara chache hujikita kwenye makosa yao wenyewe bila kusukumwa. Ukikubali kuendelea na kikao, upo tayari kujikita katika mchango wako mwenyewe kwenye tatizo ukifika wakati wako kufuata zile hatua na kuachana na matarajio ya yale ambayo mwenzako itampasa kuyaungama? Kama mwenzako hataibua jambo ambalo ni muhimu kwako, tutalishughulikia katika kikao kijacho"

**Hatua ya 3:** *Utangulizi kuhusu tiba ya msamaha na uamuzi ya kwamba inaendelea au la.* Kwa kawaida inafaa sana kuanza na mwanandoa ambaye ametenda kosa baya zaidi. Kila mwanandoa ni lazima aweke maamuzi katika mambo machache ambayo kwayo wanataka kusamehewa. Mshauri atatambua kama wana maudhui yanayofanana. Mshauri anaweza kusema: "Kikao cha Msamaha uliopangiliwa hakifuati kila kitu kuhusu ushauri nasaha. Ukimkubalia mwanandoa kuendelea [Mwanandoa A] atafuata hatua kuanzia ya 4-12 katika mtiririko, na kisha atampa nafasi [Mwanandoa B] aendelee (mshauri nasaha anaweza akachapa na kukabidhi nakala ya hatua kwa muhutasari na kwa ufupi). Nitahusika kikamilifu katika kikao, kutunza kikao kifuate mwelekeo sahihi na kwa msaada wako, na kufanya maamuzi, kwamba ni maelezo yapi ni ya kufaa katika kikao cha msamaha na nini kiwekwe kama kumbukumbu kwa wakati unaofuata."

**Hatua ya 4:** *Tamko lenye makosa.* Mwanandoa ni lazima aeleze kwa wazi tabia yao inayoumiza. Inahitaji kuelezwa kwa namna ambayo inaonyesha ufahamu kuwa lilikuwa ni kosa, linaumiza na kwamba haikuwa haki. Mara nyingi mwanandoa anaweza akahusisha katika tamko lake kitu fulani kuhusu matendo ya mwanandoa mwenzake. (k.m., mwanaume hutafuta msamaha kwa maneno akimkosoa mke wake kwenye hadhara kwa sababu asili yake ya makosa na isiyovumilia). Akihusisha mtazamo wake juu ya matendo ya mke wake hupunguza uwezo wake na kuongeza utetezi kwa upande wa mke wake. Mshauri kwa hiyo ni lazima amsaidie mwanandoa kuhusisha sehemu yake tu ya tatizo. Inasaidia kumwuliza mwanandoa, Je kosa hili lilikuwa baya?" Kama mwanandoa akisita, mshauri anapaswa kuibua hilo na kumfanya mwanadoa au kulikubali hilo kosa na kuonyesha kuwa anaamini ni baya, au kulifikiria tena. Katika visa vingi, maelezo ya kosa yanaweza kuibua mengine yaliyokuwepo.

**Hatua ya 5:** *Mkosaji anatoa maelezo.* Mshauri anaanza hatua hii kwa kuruhusiwa na mtu aliyekosewa kujaribu kujua sababu za kosa la mwenzi wake (kupata ruhusa kunamhusisha mwenzi aliyekosewa kama muhusika aliye macho kutambua tabia iliyosababisha maumivu). Mshauri anaweza akaeleza wazi kwamba baadhi ya makosa kwenye ndoa yana maelezo, lakini maelezo hayo wakati mwingine yanapotezwa kwa sababu ya majeraha au maumivu yaliyopatikana kwa pande zote mbili. Mshauri atoe tahadhari kwamba maelezo hayo yasiwe kama "utetezi" lakini ni sehemu ya kutafuta habari itakayotuwezesha sisi kufanya tathmini ya kina ya kosa. Kutafuta sababu zilizosababisha kosa inaweza kutufikisha kwenye kutambua hali tabia zilizokuwepo kabla ya kuoana. Hili, hatimaye, inaweza kusababisha wanandoa, kuwa na ufahamu mkubwa, na kuhurumiana, kila mmoja wao.

**Hatua ya 6:** *Maswali na majibu juu ya kosa.* Wanandoa wanatakiwa kujitahidi kufahamiana wao kwa

wao. Hata hivyo, maswali mengi wanayouliza yanatumika "kutafuta kueleweka" kuliko kutafuta kuelewa na kuibua taarifa. Mshauri anaweza kusema: "Kama inavyoonekana kuwa jambo la kustaabisha, mara chache wanandoa hupata majibu sahihi kwa maswali yao kwa sababu ya uwepo wa mazingira ya kujitetea dhidi ya kosa. Maswali huulizwa kwa ukali au huulizwa kwa namna ya kujitetea. Huu ni wakati wa kupata taarifa kutoka katika roho ya upendo. Embu tufanye kazi kwa pamoja ili kuelewa kwa hakika tatizo hili kwa njia ya kuuliza maswali. [Mwandoa B] una swali lolote kwa [mke/mume] wako?" Kutoa majibu na ukweli ni kumsafisha mkosaji na kuleta wepesi katika kusamehe. Mshauri anaweza kuchukua nafasi yenye umuhimu mkubwa kikamilifu katika kusaidia kuunda maswali na kuwaweka wanandoa katika mwelekeo sahihi.

**Hatua ya 7:** *Mtu aliyekosewa hutoa mwitikio wa kihisia.* Ukaribu unaweza kuja tu ikiwa mwanandoa ataweza kuungana katika hatua ya hisia. Mtu aliyekosewa anataka mkosaji asikie na kuelewa maumivu na hisia lakini anaweza kuwa na ugumu katika kuelezea hisia zake. Hapo tena, msahauri anatakiwa ahusike katika umuhimu mkubwa kusababisha nia isi-yojitetea. Mshauri anaweza kusema: "Ingawa inaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya [Mwanandoa B] kueleza maumivu yake inaweza kuwa vigumu kwa sababu anaogopa kuumiza moyo wako, je wewe [Mwanandoa A] utampa ruhusa aeleze moyo wake kikamilifu kwako kuhusu maumivu yake?" (Mwanadoa anapotoa ruhusa kwa mwingine kuelezea hisia zake, wanahama kutoka kwenye hali kujitetea binafsi na kuwa katika hali ya kupokea.) Mwanandoa aliyekosewa anaweza kueleza alivyoumia kwa wakati ule na jinsi anavyojisikia sasa baada ya kujifunza katika kipindi cha ushauri.

**Hatua ya 8:** *Mkosaji anaonyesha huruma na majuto kwa ajili maumivu aliyosababisha kwa mwenzake.* Mkosaji kueleza ipasavyo maumivu na huzuni hutoa utambuzi kwamba mateso ya mwanandoa yameeleweka na kutambuliwa. Hili, hatimaye, inatufikisha kwenye huruma na husaidia katika kuleta msamaha wa kihisia. Wanandoa wengi wanaweza kuwa wabinafsi sana na kuwa vigumu kuhisi au kuelezea huruma zao kwa mwingine. Mshauri anaweza akasaidia kwa kuuliza swali kama, "Wakati mke wako aliposema ameumia sana kwamba aliamka akilia usiku, unapofikiri hilo unapata hisia kama ipi?" Mshauri anaweza kumwomba kila mwanandoa aseme kwa muhutasari *majuto* na huruma iliyoelezwa na mwenzake.

**Hatua ya 9:** *Mkosaji anaandaa mpango kukomesha/kuzuia tabia.* Ili mtu atafute msamaha katika kweli ina maana kwamba mkosaji anapanga kukomesha tabia inayosababisha kosa na kuzuia isitokee tena siku za mbeleni. Msamaha unawezeshwa pale ambapo tendo la kurekebisha limepangwa na mfumo wa uwajibikaji umewekwa. Mpango unahitaji kuwa mahususi na uwe umewekwa na mkosaji kwa msaada wa mwenzi wake na mshauri. Mshauri anaweza kumwomba Roho Mtakatifu kuleta mawazo kwenye ufahamu na anaweza kusema: "Kwa nini tusianze na mambo ambayo unataka kujitoa kuyafanya, na labda unaandaa mawazo ambayo yatakuhakikishia kuona kwamba unajitoa kuyaishi hayo?" Mshauri anaandaa kumbukumbu ya maandishi ya kila upande wa mpango na kuhimiza umuhimu wa wanandoa kutunza mpango ulioandikwa mahali panapofikika na salama.

**Hatua ya 10:** *Mwanandoa aliyekosewa ananyesha huruma kwa ajili ya moyo wa mkosaji ulioumia.* Matatizo ya ndoa mara zote yanahusisha maumivu yanayoonekana kwa mkosaji na vile vile kwa aliyekosewa. Tabia ya mkosaji inaweza kwa sehemu ikaelezwa na maumivu yaliyopita katika mahusiano na/au maumivu yalijitokeza huko nyuma. Zaidi, mkosaji ni lazima sasa ashughulike pia na aibu na hatia ya kumsababishia maumivu kwa mwenzi wake. Mshauri anaweza kusema kwa mwenzi aliyekosewa: "Nimetambua kosa la mke wako limesababisha maumivu makubwa kwako, lakini sasa tunaona hata yeye anaumia. Unaweza kuweka katika maneno maumivu anayopitia?" Kama katika hatua ya 8, mshauri anaweza akasaidia mwenzi kupata ufahamu wa huruma.

**Hatua ya 11:** *Msisitizo kwenye uchaguzi na kujitoa kuachilia.* Mshauri anawakumbusha wanandoa mjadala wa hatua ya 1 kuhusu upendo na msamaha na kusamehe kwa kufanya maamuzi. Kama mwenzi aliyekosewa akichagua kusamehe, yeye anajitoa kimakusudi kuachilia kosa na bila kulitumia kama silaha siku za mbeleni. Hiyo haimaanishi kulazimika kuacha kuongelea tatizo; kwa hakika, kulifanyia kazi tatizo katika ushauri kunaweza kuhitajika mjadala. Kwa hiyo ni lazima mjadala ufanyike kuhusu namna ya kuzuia kucheua kosa na namna ya kushughulika na mawazo ya kulipiza kisasi ambayo yanaweza kujitokeza huko mbeleni (tazama mjadala kuhusu kujitoa hadharani kusamehe na kushikilia msamaha katika sehemu ya V. "Msamaha na Upatanisho," hapo juu).

**Hatua ya 12:** *Kuomba msamaha kirasmi.* Ili msamaha uwe wazi, wenzi wanatakiwa watamke maneno ombi na utoaji wa msamaha. Mshauri anaweza akasema: "Sasa ni wakati, kama [Mwenzi A] yupo tayari, kwa ajili ya yeye kuomba msamaha mbele yangu kama shahidi. [Mwenzi B] kisha ataitika kama yeye atatoa

Hakimiliki © 2007-20147 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

msamaha au la.” Kuomba msamaha rasmi mbele ya shahidi inakazia kwamba uamuzi thabiti umefanyika kwa ajili ya msamaha. Wanandoa wengi wanaweza kulia, kushikana mikono, au kupiga magoti kusisitiza toba yao na majuto yao juu ya kosa. Baada ya msamaha kutolewa, mshauri anaandika tarehe kamili na muda na kuwaomba wanandoa waandike mahali maalumu. Mshauri anaweza kusema: “Msamaha ulitafutwa na kutolewa mnamo saa 11:32AM katika tarehe hii. Tafadhali kumbuka zingatia kuweka kumbukumbu tarehe hii na muda kwa sababu ni takatifu katika macho ya Mungu. Kama kuna maswali kuhusu uliomba au ulitoa msamaha, tafadhali kumbuka muda na tarehe au jisikie huru kunipigia simu mimi kama shahidi.”

**Hatua ya 13:** *Tendo la kusherehekea.* Tendo la nje, la kusherehekea kati ya wanandoa litakazia msamaha walioshiriki na husaidia kufanya maamuzi yao kuwa imara na ya kudumu kiufahamu, kihisia na kiroho. Mshauri anaweza kuuliza: “Unawezaje kusherehekea msamaha uliotokea hapa—jambo litakalowakilisha msamaha kama ishara—jambo la kisherehe?” Wanandoa wanaweza kuandika makosa yao kwenye karatasi na kuchoma hayo makaratasi, kupanda mti maalumu, kuandika na kupeana barua za mapenzi, kupeana zawadi, au kufanya jambo lingine lolote litakaloweka alama kwenye msamaha wao na mwanzo wa maisha mapya pamoja. Hatua hii nzima inaweza kuwa ya kiukombozi, inayobadilisha uzoefu wa maisha unaoathiri mtu binafsi, unaoathiri mahusiano katika ndoa, na kuwaleta karibu pamoja katika kuongezeka kwa ukaribu wao kwa Kristo.

**MWANDISHI**



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipata B.A. yake katika Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, na kuibuka na daraja la juu la heshima, mwaka 1974, na kuingizwa katika jamii inayoheshimika ya Phi Beta Kappa. Kisha akapokea J.D. kutoka Cornell Law School, magna cum laude, mwaka 1977, na akawa miongoni mwa Jamii ya Sheria inayoeshimika ya Coif. Alitumia miaka 28 inayofuata akijihusisha na shughuli za sheria, kama wakili wa sheria anayejitegemea kule Chicago na baadaye kama mdau Kitengo cha sheria cha Menn Law Firm kule Appleton, WI. Mwaka 1982 akaamini na kuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Upendo wake unaokua katika theolojia ulimfanya ahitimu shahada yake ya pili katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School kule Deerfield, IL. Akahitimu shahada ya pili ya theolojia kutoka TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa Mkurugenzi wa Equipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa Equipping Church Leaders-East Africa (ECLEA). Machapisho yake yaliyosheheni ya masomo ya Biblia yanapatatikana kwenye **www.eclea.net**. Jonathan anaweza kuandikiwa au kuwasilana naye kupitia barua pepe hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.